# MATUMIZI YA UTANZIA KATIKA RIWAYA PENDWA YA KISWAHILI: ULINGANISHO WA RIWAYA ZA BEN MTOBWA NA HUSSEIN TUWA

Na

Kuruthumu Salumu Shomary Mazongela

Tasnifu kwa Ajili ya Kukamilisha Mahitaji ya Shahada ya Udhamili katika Fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dodoma.

Chuo Kikuu cha Dodoma

Oktoba,2016

**ITHIBATI**

**YA**

**MSIMAMIZI**

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma kazi hii na anapendekeza kuwa Chuo Kikuu cha Dodoma kikubali kupokea tasnifu hii: **Matumizi ya Utanzia katika Riwaya Pendwa za Kiswahili: Ulinganisho Ben Mtobwa na Hussein Tuwa,** kwa ajili ya tuzo ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili.

________________________

Dkt. A. S. PONERA
(Msimamizi)

Tarehe: ______________________

**ITHIBATI**

**NA**

**HAKIMILIKI**

Mimi, **Kuruthum Salumu Shomary Mazongela,** ninathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Umahiri au Shahada nyingine yoyote.

Saini ……….........…………

Kuruthumu Mazongela.

Tarehe ........................

Hairusiwi kunakili, kuzalisha, wala kusambaza sehemu yoyote ya tasnifu hii kwa yeyote bila kibali cha maandishi kutoka kwa Mwandishi au Chuo Kikuu cha Dodoma.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa ningependa kumshukuru Mungu kwa kuwa nami kipindi chote cha masomo yangu, pia kwa kuniwezesha kukamilisha kazi hii.

Pia, ningependa kutoa shukrani zangu za pekee kwa msimamizi wangu wa tasnifu hii, Dkt. A. S. Ponera, wa Chuo Kikuu cha Dodoma kwa ushauri wake katika hatua zote za uandishi wa kazi hii mpaka nilipoikamilisha. Aidha, kujitoa kwake kwa hali na mali katika kufanikisha uandishi wa tasnifu hii. Asante sana Dkt Ponera. Aidha, shukrani za pekee ziwaandee wahadhiri wangu Dkt. Self Khatibu, Dkt. Rafiki Sebonde na Dkt. Zuhura Badru.

Pia, ninatoa shukrani za dhati kwa wazazi wangu, marehemu baba yangu mpendwa, mzee Salum Shomary Mazongela Mungu amlaze mahali pema peponi. Mama yangu mzazi, Rehema Mrisho Tuli, kwa uvumilivu wake hasa kipindi chote cha makuzi yangu. Pia, kaka na dada zangu pamoja na mdogo wangu wa pekee, Mwanaisha Salum Mazongela, kwa kunishauri na kunitia moyo muda wote wa masomo na katika hatua za uandishi wa tasnifu hii.

Aidha, shukrani za dhati zimuendee mume wangu, Abdallah Abduly Ibrahim kwa kunisaidia na kunivumilia. Pia, watoto wapendwa Abbakary Mahenge na Abduly Abdallah kwa uvumilivu waliokuwa nao kipindi chote nilipokuwa nafanya utafiti huu. Pia, shukrani za dhati ziwaendee wanafunzi wenzangu Martina Duwe, Bisibo Taufiq, Happy Bitababaje, Harua Mohamed na Grace Mbwambo.

Kama itajitokeza dosari yoyote katika kazi hii, ninaomba ielekezwe kwangu na si kwa mtu mwingine yeyote kati ya hao niliowataja au wengineo.

# TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa wazazi wangu wapendwa, marehemu baba yangu mzazi, mzee Salum Shomary Mazongela, baba yangu mlezi, Mzee Juma Shomary Mazongela na mama yangu Rehema Mrisho Tuli kwa kunisomesha toka darasa la kwanza hadi Chuo Kikuu.

# IKISIRI

Tasnifu hii ilijigeza katika kuchunguza matumizi ya utanzia katika riwaya pendwa za Kiswahili ulinganisho wa riwaya za Ben Mtobwa na Hussein Tuwa. Ponera (2014) anasema kuwa utanzia ni mbinu ambayo mtunzi hutumia vipengele mbalimbali vizuavyo huzuni, masikitiko, jitimai na mateso kwa hadhira yake. Vipengele hivyo huweza kujengwa na mateso, ugumu wa maisha, vifungo, mabaa kama vile njaa, gharika, kimbunga, magonjwa, ulemavu (wa viungo au michakato ya mwili, pamoja na ule wa mifumo ya mwili kama vile ugumba, utasa).

Mapitio yaliyotumika katika tasnifu hii yaligawanyika katika makundi mawili. Kundi la kwanza, mapitio yanayohusiana na utanzia, na kundi la pili, mapitio yanayohusiana na riwaya pendwa. Mbinu iliyotumika ni udurusu maktabani pamoja na usaili. Maeneo yaliyotumika kukusanyia data ni Dodoma na Dar es Salaam. Nadharia iliyotumika ni uhalisia ambayo huchunguza utokeaji wa matukio ambayo huendana na hali halisi ya ulimwengu.

Matokeo ya tasnifu hii yanaonesha kuwa utanzia upo katika kazi mbalimbali za fasihi yaani, fasihi simulizi na fasihi andishi. Aidha, yanaonesha kuna aina tatu za utanzia ambazo, ni utanzia wa kimwili, utanzia wa kisaikolojia na utanzia wa kimaumbile. Pia, kuna vijenzi mbalimbali ambavyo vinaibua utanzia katika riwaya teule na jamii kwa ujumla. Vilevile, matokeo ya tasnifu hii yanaonesha kuwa kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya matukio ya kitanzia na matukio ya kifutuhi. mpya wa kitaaluma katika fasihi ya Kiswahili kama ifuatavyo: Mosi, kubainika kwa tofauti ya tanzia na utanzia. Pili, kuibuliwa kwa matukio ya utanzia ambayo hujitokeza katika riwaya pendwa na si tamthiliya pekee. Tatu, kuibuliwa kwa aina mbalimbali za utanzia zilizotumika na waandishi teule.

# YALIYOMO


ITHIBATI YA MSIMAMIZI ........ i

ITHIBATI NA HAKIMILIKI ........ ii

SHUKRANI ........ iii

TABARUKU ........ iv

IKISIRI ........ v

YALIYOMO ........ vi

VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA ........ x

**SURA YA KWANZA ........ 1**

**UTANGULIZI ........ 1**

1. 1 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu Zilizotumika ........ 1

1. 1. 1 Riwaya ........ 1

1. 1. 2 Riwaya Pendwa ........ 1

1. 1. 3 Tanzia ........ 3

1. 1. 4 Utanzia ........ 5

1. 1. 5 Uhusiano wa Utanzia na Ufutuhi ........ 7

1. 2 Usuli wa Tatizo la Utafiti na Tamko la Tatizo la Utafiti ........ 8

1. 2. 1 Usuli wa Tatizo la Utafiti ........ 8

1. 2. 2 Tamko la Tatizo la Utafiti ........ 14

1. 3 Malengo ya Utafiti ........ 14

1. 3. 1 Lengo kuu ........ 14

1. 3. 2 Malengo Mahususi ........ 14

1. 4 Maswali ya Utafiti ........ 14

1. 5 Manufaa wa Utafiti ........ 15

1.6 Taarifa Fupi za Waandishi Teule ........ 15

1. 6. 1 Taarifa Fupi ya Ben Mtobwa ........ 15

1. 6. 2 Taarifa Fupi ya Hussein Tuwa ........ 17

1. 7 Upeo wa Utafiti ........ 18

1. 8 Muhtasari wa Sura ya Kwanza ........ 19

**SURA YA PILI ………………………………………………………………20**
**KIUNZI CHA NADHARIA NA MAPITIO YA MAANDIKO ........................... 20**
2. 1 Utangulizi ......................................................................................... 20
2. 2 Kiunzi cha Nadharia ya Utafiti ......................................................... 20
2. 3 Mapitio ya Maandiko ......................................................................... 25
2. 3. 1 Maandiko Yanayohusu Utanzia ..................................................... 25
2. 3. 2 Maandiko kuhusu Riwaya Pendwa ................................................ 27
2. 4 Mapengo Yaliyojitokeza ..................................................................... 29
2. 5 Muhtasari wa Sura ya Pili .................................................................. 29

**SURA YA TATU……………………..……………………………………….30**
**METHODOLOJIA YA UTAFITI ......................................................... 30**
3. 1 Utangulizi ......................................................................................... 30
3. 2 Mpango wa Utafiti ............................................................................ 30
3. 3 Eneo la Utafiti ................................................................................... 30
3. 4 Walengwa wa Utafiti ......................................................................... 31
3. 4. 1 Jamii ya Wafitiwa .......................................................................... 31
3. 4. 2 Sampuli ya Watafitiwa na Upatikanaji Wake ................................ 31
3. 5 Ukusanyaji wa Data .......................................................................... 32
3. 5. 1 Njia na Zana za Kukusanyia Data ................................................. 32
3. 5. 2 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data na Udhibiti wake .................... 32
3. 6 Uchanganuzi wa Data ........................................................................ 33
3. 7 Itikeli za Utafiti ................................................................................. 33
3. 8 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti ....................................... 33
3. 9 Vikwazo vya Utafiti .......................................................................... 34
3. 10 Muhtasari wa Sura ya Tatu ............................................................. 34

**SURAYA NNE.........................................................................................35**
**MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI ............................................ 35**
4. 1 Utangulizi ......................................................................................... 35
4. 2 Vipengele Vinavyobainisha Utanzia katika Riwaya Teule ................ 35
4. 2. 1 Vijenzi vya Utanzia ........................................................................ 35
4. 2. 1. 1 Vifo ............................................................................................ 35
4. 2. 1. 2 Vifungo ....................................................................................... 36

4. 2. 1. 3 Magonjwa.......... 37
4. 2. 1. 4 Ugumu wa Maisha .......... 38
4. 2. 1. 5 Ulemavu wa Viungo .......... 38
4. 2. 1. 6 Ukatili.......... 39
4. 2. 1. 7 Ajali.......... 40
4. 2. 1. 8 Mabaa Makubwa.......... 41
4. 2. 2 Aina za Utanzia.......... 41
4. 2. 2. 1 Utanzia wa Kisaikolojia.......... 42
4. 2. 2. 2 Utanzia wa Kimwili .......... 43
4. 2. 2. 3 Utanzia wa Kimaumbile.......... 44
4. 3 Utanzia katika Riwaya za Waandishi Teule.......... 45
4. 3. 1 Riwaya Teule za Ben Mtobwa .......... 45
4. 3. 1. 1 Muhtasari wa Riwaya ya *Najisikia Kuua Tena*.......... 45
4. 3. 1. 2 Muhtasari wa Riwaya ya *Dimbwi la Damu* .......... 46
4. 3. 2 Matukio ya Kitanzia katika Riwaya za Ben Mtobwa.......... 47
4. 3. 2. 1 Matukio ya Kitanzia katika Riwaya ya *Najisikia Kuua Tena*.......... 47
4. 3. 2. 2 Matukio ya Kitanzia katika Riwaya ya *Dimbwi la Damu*.......... 51
4.3.3 Riwaya Teule za Hussein Tuwa.......... 56
4. 3. 3. 1 Muhtasari wa Riwaya ya Mkimbizi.......... 56
4. 3. 3. 2 Muhtasari wa Riwaya ya Mdunguaji .......... 56
4. 3. 4 Matukio ya Kitanzia katika Riwaya za Hussein Tuwa .......... 57
4. 3. 4. 1 Matukio ya Kitanzia katika Riwaya ya Mkimbizi .......... 58
4. 3. 4. 2 Matukio ya Kitanzia katika Riwaya ya Mdunguaji.......... 62
4. 4 Kufanana na Kutofautiana kwa Utanzia Uliomo katika Riwaya za Waandishi Teule.......... 65
4. 4. 1 Kufanana kwa Utanzia Uliomo katika Riwaya za Waandishi Teule. .......... 66
4. 4. 1. 1 Kufanana kwa Aina za Utanzia.......... 66
4. 4. 1. 2 Kufanana kwa Malengo ya Utanzia .......... 68
4. 4. 2 Kutofautisha Utanzia katika Riwaya za Waandishi Teule.......... 70
4. 4. 2. 1 Tofauti ya Idadi ya Matukio ya Kitanzia .......... 70
4. 4. 2. 2 Tofauti ya Kimtazamo.......... 70
4. 4. 4 Muhtasari wa Sura ya Nne .......... 71

**SURA YA TANO ……………………………………………………………………72**
**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO........................................... 72**
5. 1 Utangulizi......................................................................................... 72
5. 2 Muhtasari ......................................................................................... 72
5. 3 Hitimisho.......................................................................................... 73
5. 3. 1 Utoshelevu wa Mkabala Uliotumika katika Utafiti ........................................ 73
5. 3. 2 Mchango Mpya wa Utafiti ..................................................................... 74
5. 4 Mapendekezo ya Tafiti Zijazo ................................................................. 74
MAREJELEO ......................................................................................... 76
VIAMBATISHO....................................................................................... 80

## VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

| | |
|---|---|
| Bi | Bibi |
| Dkt | Daktari wa falsafa |
| ed | *edition* |
| http | *Hyper Text Transfer Protocal* |
| Ltd. | *Limited* |
| MBA | *Master of Business Administration* |
| nd | *Second* |
| Prof. | *Professor* |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| Uk | Ukurasa |
| USA | *United State of America* |
| UWAKI | Ukatili wa Kijinsia |
| www | *World Wide Web* |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1. 1 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu Zilizotumika

### 1. 1. 1 Riwaya

Wamitila (2003:178) anasema kuwa riwaya ni kazi ya kinathari au kibunilizi ambayo huwa na urefu wa kutosha, msuko uliojengeka vizuri, wahusika wengi walioendelezwa kwa kina, yenye kuchukua muda mwingi katika maandalizi na kuhusisha mandhari maalumu. Kwa jumla, tunaweza kusema kwamba, riwaya ni kazi ya kubuni au ya kinathari inayoakisi matukio fulani katika jamii fulani. Ni hadithi yenye urefu wa kutosha na matukio yake yamejengwa na wahusika wanaowakilisha utamaduni wa jamii husika.

### 1. 1. 2 Riwaya Pendwa

Madumulla (2009) anasema kuwa, riwaya pendwa ni riwaya ambayo inajihusisha na masuala ya mapenzi, upelelezi na ujasusi ambapo mara nyingine katika ufuatiliaji wake kuna mapigano makali ya kimwili au kiakili kati ya mtu mmoja au wachache na watu wengi. Matokeo yake ni kwamba mtu mmoja anawashinda walio wengi. Riwaya ya kisasa inaoana sana na maisha mapya ya kisasa. Suala linalowasumbua hasa watu wanaokabili maisha ya kidemokrasia ni namna gani na jinsi gani ya kuishi. Hilo suala muhimu linaulizwa na kuchanganuliwa kwa urahisi zaidi na moja kwa moja katika muundo na wa riwaya kuliko tanzu nyingine za fasihi (Nakano, 1961).

Riwaya ya pendwa ilizuka huko ulaya katikati ya karne ya kumi na nane. Kuzuka kwa riwaya kulisababishwa na mabadiliko ya kijamii. Senkoro (1987) anasema kuwa

riwaya ni utanzu wa fasihi ambao kuzuka kwake kulifungamana na kuzuka kwa ubepari. Miji na viwanda ni mazao ya ubepari.

Ubepari huu ulifungana na mapinduzi ya viwanda ambayo yalitokea katika karne ya kumi na nane huko Uingereza. Mapinduzi haya yalileta nyenzo mpya kama mashine ya kurahisisha kazi na vyombo vya usafiri kama vile meli na treni. Nyenzo hizi ziliwafanya mafundi wa kazi za mikono waache kazi hizo na kukimbilia kuajiriwa viwandani. Wakulima wadogo wadogo nao walilazimika kuhamia mijini ili waweze kujinufaisha na mfumo huu mpya wa maisha.

Kabla ya karne ya kumi na nane mfumo wa kijamii ulikuwa wa utawala wa kifalme na kikabila ambao uliongozwa na imani ya Mungu kupitia madhehebu mbalimbali. Kukua kwa viwanda kuliwezesha tabaka jipya la mabepari kujiimarisha na hatimaye kuwa na madaraka kamili ya kuongoza mfumo wa kijamii. Mapinduzi ya Marekani ya 1776 na yale ya ufaransa ya 1789 yalikuwa ni vielelezo vya ushindi wa tabaka la mabwanyenye dhidi ya makabila na mamwinyi.

Uhusiano uliopo kati ya uzukaji wa ubepari na maendeleo ya riwaya unajidhihirisha wazi. Tabaka hili jipya la mabepari halikuwa na haki ya kurithi kama ilivyokuwa kwa wafalme, makabaila na watu wa nasaba bora, bali kwa ari kubwa walipata mali kwa akili zao wenyewe pamoja na jitihada zao. Watu wa tabaka hili hawakuridhika na fasihi rasmi ya wakati huo ambayo wahusika wake wakuu walikuwa ni watu wa nasaba bora na maudhui yake yalihusu ujasiri na mapenzi ya watu wakubwa tu. Walitamani kusoma hadithi zinazowahusu watu wa kawaida, hadithi zinazogusa hisia zao na kudokezea namna ya kuishi na kupata maendeleo katika kipindi hicho kilichoshuhudia mabadiliko ya haraka sana yaliypotokana na mavumbuzi mapya yaliyokuwa yakifanywa. Hivyo, matabaka mapya ya mabepari na wafanyakazi

yalihisi kwamba yametunukiwa zawadi kubwa kwa kupata riwaya ya uhalisia inayosawiri maisha yao wenyewe.

Riwaya hii ya kisasa ilikuwa tofauti na visasili au utendi. Wakati maisha ya utendi yalilenga maisha ya nchi au makabaila au jamii kwa ujumla, riwaya ya kisasa yenye mwelekeo wa "uhalisia" ilizungumzia maisha ya kawaida ya mtu binafsi na ilizingatia na kusisitiza "umimi." Pamoja na maudhui, fani ya riwaya ya kisasa pia ilikuwa tofauti. Riwaya ilichagua mtindo wa kinathari usiofungwa na sheria au kanuni za lazima kama zilizotawala fasihi ya urasimi. Mtindo huu ulikuwa huru na uliweza kunyambulika na kulingana na wakati na utamaduni wa jamii. Hisia za mwandishi au mchomo na jazba zake zilipewa aula katika utungaji wa riwaya.

Riwaya ya kisasa inayodhaniwa kuwa ya kwanza kabisa katika fasihi ya Kiingereza ni ile ya *Pamela* iliyoandikwa na Samuel Richardson na kuchapishwa mwaka 1740, ni kielelezo kizuri cha fani hii mpya. Riwaya hii iliandikwa kinathari na kihalisia katka mtindo wa barua, na ilisawiri kwa dhati hisia za mhusika wake mkuu ambaye ni mjakazi wa tabaka la chini aliyeitwa Pamela. Misingi hii iliyowekwa na riwaya ya mwanzo ndiyo iliyofuatwa na riwaya pendwa ambayo ilizuka katika karne ya kumi na nane.

### 1. 1. 3 Tanzia

Tanzia kama kipera kimojawapo cha fasihi andishi kimeanza zamani sana katika utanzu wa tamthiliya. Kwa mujibu wa *Oxford advanced learner,s dictionary* (2006:1569), neno tanzia, limeelezwa kwa namna mbili kama ifuatavyo: *Tragedy is a very sad event or situation, especially one that involves death or tragedy is a serious play with a sad ending, especially one in which the main character dies*. Yaani, tanzia ni tukio au hali ya kusikitisha sana, ambalo hasa huhusisha kifo au tanzia ni

mchezo makini ambao mwishoni ni huzuni. Fasili hii ina mambo muhimu mawili yanayohusu tanzia mambo hayo ni kuwepo kwa huzuni ndani yake kama lengo kuu, pamoja na kuwepo kwa uhusiano wa tanzia na utanzu wa tamthiliya. Hivyo, chimbuko la tanzia hasa limo katika utanzu wa tamthiliya. Akifafanua zaidi kuhusu tanzia kama utanzu mmojawapo wa tamthiliya, Wamitila (2002) anasema kuwa;

> Tanzia ni aina ya tamthiliya ambayo huwa na suala la matendo na malengo dhati. Utanzu huu kama 'mwigo' au 'uigaji' wa tendo ambalo lina udhati, ukamilifu, ubora na ukuu fulani. Tendo hilo lazima liwe na uwezo wa kuwaathiri watazamaji na kuwafanya waingiwe na huzuni au kihoro pamoja na kuwa na uwezo wa kuzitakasa hisia za woga au huzuni (uk. 76).

Hoja hii ya Wamitila inabainisha undani wa tanzia na kubainisha kuwa kuna matendo yaliyo dhati ndani yake. Yaani ni matendo halisi yanayoigwa kutoka kwa binadamu. Matendo hayo ndio yanayoibua hali ya huzuni pamoja na woga.

Chimbuko la dhana ya tanzia ni katika jamii ya Kigiriki. Tanzia, ambayo kwa lugha ya Kiingereza '*Tragedy'* ilitokana na neno *tragōidia* la lugha ya Kigiriki, au "mbuzi-wimbo," kutoka *Tragos* ("mbuzi") na *aeidein* ("kuimba"). Neno lenyewe linaweza kuwa linajulikana ama kwa tuzo. Na kwamba mbuzi alikuwa tuzo kwa mchezo ambao mtu alishinda mashindano ya mwanzo au kwa mavazi (mbuzi ngozi) ya wasanii, au mbuzi alitolewa kafara katika mila ambayo tanzia iliendelea (Sewall, 2015).

Sewall anaendelea kusema kuwa tanzia ilianzishwa katika vipindi vinne ambavyo ni: Attica, Ugiriki, katika karne ya 5 KK; Uingereza katika utawala wa Elizabeth I na James I, 1558-1625; Karne ya 17 Ufaransa; na Ulaya na Marekani katika nusu ya pili ya karne ya 19 na nusu ya kwanza ya 20. Mabadiliko mengi yamepitia dhana ya tanzia tangu ilipozungumzwa na Aristotle. Baadhi ya watunzi na wahakiki

wanazungumzia tanzia yenye kusawiri matumaini, tanzia hizi huhubiri matumaini licha ya misiba inayowakuta wahusika wakuu. Katika fasihi ya Kiswahili, wahusika hawa ni kama vile Kinjeketile, Mzalendo Kimathi na Mukwava. Katika kipindi cha kisasa, takribani kutoka katikati ya karne ya 19, wazo la tanzia lilipatikana katika mfano wa umbo halisi la riwaya.

### 1. 1. 4 Utanzia

Ponera (2014) anasema kuwa utanzia ni mbinu ambayo mtunzi hutumia vipengele mbalimbali vizuavyo huzuni, masikitiko, jitimai na mateso kwa hadhira yake. Vipengele hivyo huweza kujengwa na mateso, ugumu wa maisha, vifungo, mabaa kama vile njaa, gharika, kimbunga, magonjwa, ulemavu (wa viungo au michakato ya mwili, pamoja na ule wa mifumo ya mwili kama vile ugumba, utasa).

Dhana ya utanzia imetokana na dhana mama ya tanzia, yaani matukio yanayoibua huzuni au masikitiko katika tamthiliya. Utanzia katika utafiti huu unamaanisha hali ijengwayo na maneno, matukio au mazingira yoyote yenye kuwafanya watu wahuzunike, wasononeke na wasikitike. Tumeitofautisha dhana ya utanzia na tanzia kwa misingi ya kwamba, tanzia kwa kiasi kikubwa hujiegeza katika utendaji hususani matendo ya jukwaani. Wamitila (2002), anasema kuwa tendo hilo lazima liwe na uwezo wa kuwaathiri watazamaji na kuwafanya waingiwe na huzuni au kihoro pamoja na kuwa na uwezo wa kuzitakasa hisia za woga au huzuni katika kile kinachoitwa mtakasohisia. Lakini, utanzia siyo lazima ujitokeze katika matendo ya jukwaani pekee. Hivyo, utanzia huweza kujitokeza katika tanzu mbalimbali za fasihi hata zile zilizo nje ya utanzu wa tamthiliya kama vile ushairi, riwaya na kumbo nyingine za fasihi.

Soileau (2006) anatoa ufafanuzi kuhusiana na tofauti iliyopo kati ya tanzia na utanzia kama anavyosema:

> *It is common to point out a distinction between the words 'tragedy' and the 'tragic'. 'Tragedy' in such a discussion usually refers to the literary form of a work, normally a drama but here a novel, which presents an interpretation of the meaning of human life or suffering and arouses a particular emotional response. 'Tragic' refers to a particular way of looking at the world...that tragic form in literature is a culture trait that can be spread by diffusion throughout the literary world to the point that it becomes a common and shared way of interpreting certain aspects of our existence* (uk. 4-5).
>
> Kuna tofauti ya wazi kati ya neno "tanzia" na "utanzia". Tanzia ni kazi ya fasihi hasa katika tamthiliya na kwa sasa inajitokeza katika riwaya, ambayo inatoa maana halisi ya maisha ya mwanadamu au mateso (anguko) pamoja na kuibua hisia fulani. Wakati "utanzia" ni namna fulani ya kuitazama dunia… kwamba utanzia ni mbinu ya kisanaa inayoonesha tabia ya kiutamaduni inayoenea katika dunia ya fasihi inayojulikana na kuhusiana na taratibu za maisha ya jamii (tafsiri ya Mtafiti)

Maelezo ya mtaalamu huyu yanatoa ufafanuzi mzuri wa kupata uelewa wa kuwapo kwa tofauti kati ya dhana ya tanzia na utanzia. Tanzia kwa mujibu wa mtaalamu huyu ni aina ya tamthiliya inayohusu masuala ya mateso. Suala la mateso hutoa hisia za kuhuzunisha kwa msomaji na mtazamaji wa tamthiliya. Kwa upande wa utanzia, hii ni mbinu ya kisanaa katika kutazama dunia kutokana na mambo mbalimbali yanayotokea katika utamaduni fulani. Mambo ambayo huibua hali ya huzuni katika jamii husika.

Hoja ya kuwapo kwa uwezekano wa kupatikana kwa utanzia katika riwaya inatokana na Bakhtin (1981) anayesema kuwa, utanzu wa riwaya una uwezo wa kujumlisha wasifu wa tanzu nyingine lakini ukabakia na sifa zake kama utanzu. Kwa mfano, riwaya inaweza kuhusisha kipengele cha mazungumzo ambacho kinahusishwa zaidi na tamthiliya au ikahusisha na ushairi na bado ikabakia kuwa riwaya. Mhakiki huyu anauona utanzu huu kama utanzu wa pekee kwa kuwa unazifuata tanzu nyingine,

ukabainisha ukaida wa hali zao na lugha na kuzifyonza tanzu hizo na kuzijumlisha nyingine katika muundo wake wa pekee. Andiko hili linatupa dira kuwa utanzu wa riwaya unaweza kubeba sifa za utanzu mwingine wa fasihi. Hivyo, hata utanzia ambao una sifa ya kupatikana katika utanzu wa tamthiliya unaweza kupatikana pia, katika utanzu wa riwaya

### 1. 1. 5 Uhusiano wa Utanzia na Ufutuhi

Ufutuhi na utanzia huongozana kwa sababu huzuni yafungamana na furaha, ni pande mbili za shilingi moja. Ufutuhi ni kufurahia kitu tulichonacho ambapo utanzia ni kuumia kwa sababu tumepotewa nacho. Hivyo, maelezo hayo yanaonyesha kwamba hisia hizo mbili zinahusiana sana, ni kama mapacha wanaonyonya ziwa moja. Furaha na huzuni hufanana pia kwa namna nyingine si hisia zinazotugusa kidogo tu, zote zina uwezo wa kutushika kabisa wala hazipimiki.

Hoja ya kuwepo kwa uhusiano wa utanzia na ufutuhi unashadadiwa na Senkoro (2011) anafafanua kuwa:

> Matukio ya kitanzia hujitokeza katika fasihi simulizi na andishi. Mtambaji anapokuwa na hadhira yake huyatumia matukio ambayo husikitisha katika hali ya taharuki. Baadaye mtambaji hutumia mbinu ya ucheshi ili hadhira yake ipumue kidogo kwa kutabasamu. Hii ni baada ya kutumia matukio ya kutisha au maelezo marefumarefu yenye kuwachisha wasikilizaji (uk. 71).

Maelezo ya mtaalamu huyu yanatujuza kuwa mwandishi huweza kutumia njia ya ucheshi na huzuni kwa wakati mmoja ili hadhira inapopata hisia ya huzuni baadaye huweza kuirejesha katika hali ya ucheshi. Hivyo, dhana hizi mbili zina uhusiano wa karibu kutokana na kutegemeana katika matumizi.

## 1. 2 Usuli wa Tatizo la Utafiti na Tamko la Tatizo la Utafiti

### 1. 2. 1 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Kipindi kirefu nchini Tanzania, watunzi wa fasihi andishi hususani riwaya pendwa wamekuwa wakitunga kazi zao kwa kutumia mbinu ya utanzia, aidha kwa kujua au kutokujua. Kutokana na matukio mbalimbali yanayotokea katika jamii. Neno utanzia (*tragic)* hutumika kufafanua ukosefu wa furaha ambayo watu huhisi maishani, ukosefu huo wa furaha husababisha hali ya huzuni. Kwa sababu ni jambo la kawaida kuwa na huzuni, ni muhimu kutofautisha baina ya ukosefu wa furaha wa maisha ya kawaida na dalili za hali ya huzuni. Kuomboleza kifo cha mpendwa, kuvunja uhusiano ama kuvunja matarajio makubwa ama kukumbwa na matatizo humfanya watu wengi kukosa furaha au kuhisi huzuni. Hali hii ni ya kawaida na hukumba mtu kwa wakati fulani na huendelea kwa muda tu, huzuni inayokumba mtu ni tukio la kawaida katika maisha.

Hali ya huzuni inaonekana sana na huathiri mtu mmoja kati ya watu watano katika wakati fulani maishani mwao. Huzuni ni ya maana na ya dhiki na huhatarisha maisha na hali njema ya yule aliyeathiriwa. Aliyeathiriwa hukosa hamu ya kuishi, hukosa kufanya mambo kwa makini na nguvu na hupata mabadiliko katika hamu ya kula na mpangilio wa usingizi. Watu hawa huwa na hali ya lawama, ukosefu wa tumaini huwafanya kuwa na mawazo ya kujiua. Hali hii inawezekana kutokea kwa kupitia wakati mgumu maishani na mtu hawezi kuushinda.

Mpaka sasa utanzia unaonekana kutawala katika nyanja mbalimbali za kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Katika siasa kuna matukio mengi yanayoibua utanzia kwa jamii kutokana na shughuli zake za kisiasa. Kwa mfano, shughuli za kampeni za uchaguzi kwa ajili ya kuchagua viongozi mbalimbali wa nchi husababisha matukio

ya kitanzia kwa makusudi au kwa bahati mbaya. Aidha, katika nyanja ya kiuchumi pia, kuna matukio ya kitanzia yanayoendelea kila siku na kusababisha utanzia kwa jamii au kwa taifa. Kwa mfano, tukio la mapigano baina ya wakulima na wafugaji yanayoendelea katika mkoa wa Morogoro husababisha tanzia kila siku kwa kufanya matukio ya kuharibu uchumi wa nchi na mauaji ya wananchi. Shughuli hizi za kilimo na ufugaji ni za kuinua uchumi wa nchi lakini zinakumbwa na matukio ya kuhuzunisha kila kukicha.

Vilevile, katika suala la kijamii tunaona katika jamii ambazo bado hazijaelimika wanaendeleza ndoa za utotoni. Ndoa hizi zinasababisha hali ya huzuni kwa jamii, kwa sababu wasichana hawa huweza kubeba mimba wakiwa na umri mdogo na hatimaye, wakati wakujifungua hupoteza maisha au ya mtoto au wote kwa pamoja. Pia, katika jamii ambazo zinaendeleza suala la kukeketa wasichana. Jambo hili huweza kusababisha utanzia kwa jamii husika na kwa mhusika mwenyewe. Kwa sababu sio wote waliokuwa na utayari wa kufanyiwa jambo hili, hivyo hujikuta wakikubali kwa shingo upande. Pia, inaweza kutokea wakati wa ukeketaji ikamwagika damu nyingi na hatimaye kupoteza maisha.

Utanzia katika sanaa mbalimbali huweza kujitokeza katika uchoraji. Uchoraji ni aina ya sanaa ambayo hutumia vifaa kama vile, kalamu, brashi na kadhalika kwa ajili ya kuchora picha au michoro mbalimbali TUKI (2004). Michoro hiyo huweza kuashiria hali ya utanzia kwa jamii husika. Kwa mfano, katika maandiko matakatifu ya biblia kuna maelezo ambayo huzungumnzia mateso ya Yesu. Kutokana na maelezo hayo wasanii wameyatumia maandiko hayo kuchora picha mbalimbali zinazoashiria mateso hayo. Union Vision (1997) inasema:

> Basi ndipo Pirato alipomtwaa Yesu na kumpiga mijeledi na askari wakasokota taji la mwiba, wakamtia kichwani, wakimwendea

> wakisema salamu mfalme wa Wayahudi, wakampiga makofi.....umati mkubwa wa watu walimfuata, na wanawake walikuwa wakijipiga vifua na kuombeleza. (Yohana sura ya 18 na Luka sura ya 3)

Wasanii wametumia maneno haya kuchora picha mbalimbali zinazomuonesha Yesu akisulubiwa msalabani. Picha hizo husababisha utanzia kwa mtazamaji. Kwa mfano picha za makanisani hususani katika makanisa ya Romani Katoliki

Utanzia katika sanaa za Waswahili hujitokeza katika maeneo tofauti tofauti kama vile katika ushairi, sanaa za maonesho, filamu na nyinginezo. Katika utenzi wa Kiswahili wa Fumo Liyongo, kuna utanzia wa wazi uliojitokeza katika baadhi ya beti zake. Mwandishi anasema:

> Ametiwa kitovini,
> Shaba sindani yuwani,
> Wakamtia muini,
> Akazikwa kwa umoya uk 54.
>
> Ma'ke Liyongo hakika,
> Matanga aliyaweka,
> Watu wakasikitika,
> Kwa Liyongo kuifiya uk 57 (Mulokozi 2002).

Utenzi huo unaelezea jinsi kifo cha Fumo Liyongo. Kitendo hiki cha kuuwawa kwa Liyongo husababisha utanzia katika jamii ya Liyonngo. Hali hii ya utanzia hujitokeza pia, katika sanaa nyinginezo za Kiswahili ikiwemo riwaya pendwa.

Kutokana na matukio mbalimbali ya kitanzia yanayotokea katika jamii, watunzi hawakuwa nyuma katika kuliangalia hilo. Hivyo, kwa mara ya kwanza, ilisemekana kuwa utanzia hupatikana katika tamthiliya pekee. Jambo ambalo sio kweli kwani kutokana na kuwa fasihi ni mwigo mambo halisi yanayotokea katika jamii, utanzia pia hunajitokeza katika tanzu nyingine za fasihi ikiwemo riwaya pendwa.

Seni (2015) anaeleza kuwa utanzu wa riwaya umekuja baada ya utanzu wa ushairi na tamthiliya lakini ukuaji wake umekuwa kwa kasi kubwa. Inasemekana kwamba

riwaya ya Kiswahili ilianza kujitokeza mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Kwa nini ilichelewa sana hapa Tanzania? Sababu yake ni kwamba, hadhira kubwa ya watu haikujua kusoma na kuandika. Pili, hadhira kubwa ya watu haikuweza kununua vitabu, na Tatu, jamii ya Waswahili haikuwa na mitambo ya kupigia chapa na haikuwa na mfumo mzuri wa usambazaji wa vitabu. Hivyo, tunaona kwamba wakati wa ujio wa wakoloni ulisababisha kuanzishwa kwa baadhi ya vituo vya kupigia chapa, kwa mujibu wa Mulokozi (1996) anasema kuwa ukoloni uliweka mazingira ambayo yameweza kuilea riwaya. Kwa mfano: hati ya maandishi ya Kirumi na mfumo wa usambazaji wa vitabu. Mwanzo ni riwaya ya Kiswahili ilianza kujitokeza kwanza kama tafsiri ya kazi za nje, hivyo tafsiri nayo ilisaidia sana kuchipuka kwa riwaya. Kwa kadri tafsiri zilivyokuwa zikifanywa, Waswahili walianza kuiga vitabu hivyo.

Mwaka 1930 kulianzishwa kamati ya lugha ya Kiswahili Afrika mashariki. Kamati hiyo ilihimiza uandishi wa lugha ya Kiswahili kwa njia ya kushindana. Hivyo, ilianzisha mashindano ya uandishi wa Kiswahili. Riwaya ya kwanza ya Kiswahili ilikuwa *Uhuru wa Watumwa* ya Mbotela Ilichapishwa mwaka 1934, riwaya nyingine ni *Mzimu wa Watu wa Kale* na *Simu ya Kifo*. Mwaka 1940 hadi 1960. Kulijitokeza riwaya ambazo zilikuwa zikifuata mkondo wa kingano. Njogu na Chimerah (2008) wanaeleza kuwa kimaudhui riwaya nyingi zilikuwa na mambo ya kimila na tabia kama njia ya kutunza maadili. Miongoni mwa riwaya hizo ni *Utu Bora Mkulima, Kufikirika, Kusaidikika, Adili* na *Nduguze* na *Siku ya Watenzi Wote* zote za Shaaban Robert. Kulikuwa na mambo yafuatayo: Ukombozi wa bara la Afrika na ujenzi wa jamii mpya, hivyo maudhui yake yalikuwa ni ujenzi wa jamii mpya, kufuta ubinafsi na ukandamizaji, zilikuwa zikihakiki unyama wa maisha ya kimiji na zilikuwa zikiielekeza jamii katika mkondo wa kibinadamu katika usawa na ustawi. Mfano wa

riwaya hizo ni *Lila na Fila* na *Kaburi Bila Msalaba* zilizoandikwa na Kareithi katika kipindi hiki pia kulijitokeza kundi la riwaya pendwa zilizohusu upelelezi na uharifu, kwa mfano *Mzimu wa Watu wa Kale, Kisima cha Giningi*, *Simu ya Kifo* zile za uhalifu ni *Mtaka Yote Hukosa Yote* ya Leo Odera Omera, *Tatizo Kisauni* ya Chadhoro.

Mwaka 1970 hadi 2000 ni kipindi cha kupevuka na kushamiri kwa riwaya ya Kiswahili, katika kipindi hiki riwaya nyingi zilianza kujishughulisha na uongozi na usaliti wa kisiasa. Njogu na Chimerah (2008) wanadai kuwa, wasanii walianza kutafakari jinsi ukoloni ulivyoanza kufungua milango kwa watu wachache na kutumia mali kwa manufaa yao wenyewe. Katika kipindi hiki kuliibuka riwaya za kihistoria kwa mfano *Kwa Heri Iselamagazi* iliyoandikwa na Mapalala. *Miradi Bubu ya Wazalendo*. Katika kipindi hiki kulizuka riwaya za kifalsafa na za majaribio. Mfano *Nagona* (1987), *Mzingile* (1991) za Kezilahabi. Riwaya ya *Zilahiri na Zirani* ya William. Katika kipindi hiki kulikuwa na ongezeko la riwaya za vijana na watoto. Mfano wa riwaya hizo ni *Mashujaa wa Kaza Kamba ya Shija* (1980), *Wimbo wa Sokomoko* (1990), *Ngome ya Mianzi* (1990), *Ngoma ya Mianzi* (1991) *Moto wa Mianzi* (1995) zote hizi ni za Mulokozi.

Majaribio na mabadiliko katika riwaya ya Kiswahili, yanatokana na fasihi kuitathmini jamii kihistoria, kiitikadi, kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii, na kwa kuwa jamii imekuwa ikibadilika badilika kimtazamo, fasihi nayo imekuwa ikibadilika kwa sababu jamii inabadilika. Na hivyo fasihi nayo inahitaji kupokea mabadiliko hayo ili kuendana na jamii husika. Mabadiliko katika riwaya (fasihi) yanatokea kwa sababu ya wasanii kutumia vionjo vipya katika kuziumba kazi zao. Kama anavyosema Khamisi (2007) kuwa mara moja tunaona neno kionjo

linajisemea lenyewe kimya kimya juu ya mabadiliko ya utanzu wa fasihi. Lengo la mabadiliko hayo ni kwamba "chenye mwanzo hakikosi kuwa na mwisho". Utanzu wa riwaya ya Kiswahili haukuepuka mabadiliko. Sababu zilizopelekea mabadiliko haya ni makali ya wembe wa kisiasa, kwa mfano nchini Kenya makali ya kisiasa yalikuwa dhidi ya Masosholisti, kwa mfano riwaya ya *Gamba la Nyoka*. Majaribio na mabadiliko ya riwaya ya Kiswahili yalianza pale ambapo waandishi wengi wa Kenya na Tanzania walipoanza kukataa kuitikia hewala, kwa kila wanachosikia. Hivyo, wakaanza kuandika riwaya tofauti na za mwanzo.

Madumulla (2009) akiwanukuu Scholes na Aplloe kuwa riwaya huweza kubadilika kutokana na utanzu wenyewe kuwa hauna mashiko, legelege, tepetepe na hubadilika badilika. Hivyo, kutokana na majaribio na mabadiliko katika riwaya ya Kiswahili tunaona upya wa kazi za riwaya katika fani na maudhui yake. Kisanaa riwaya hizi zinachanganya uhalisia na falsafa, mfano wa riwaya ya *Kufikirika*. Riwaya hizi zinakuwa na mwingiliano matini yaani kuchanganya kazi nyingi katika kazi moja. Kisanaa zina wahusika wa kidhana. Pia, riwaya hizi zina mazingaombwe sana, kwa mfano katika *Nagona* lugha yake ni ya mafumbo, visasili, pia ni lugha inayoelekeza, haifafanui sana. Kimaudhui riwaya hizi za majaribio zinatazama matatizo kwa mtazamo wa ndani. Zinashughulikia masuala ya ulimwengu wote, riwaya hizi pia, kimaudhui zinaitetea dunia dhidi ya maangamizi ya uovu mkubwa.

Kwa hiyo, baadhi ya riwaya ya Kiswahili imetawaliwa na utanzia katika kueleza matatizo yanayoikumba jamii katika maisha na masuluhisho yake hususani riwaya pendwa. Kutokana na kwamba ni riwaya ambayo haifungamani na masharti ya kanuni katika uandishi wake. Hivyo basi, utanzia haupo tu katika utanzu wa tamthiliya pekee bali hupatikana katika sanaa nyingine.

### 1. 2. 2 Tamko la Tatizo la Utafiti

Baadhi ya maandiko mbalimbali yaliyopitiwa yanaonesha kuwa mbinu ya utanzia, imezoeleka katika tamthiliya pekee na siyo katika riwaya. Kwa hiyo, kutofanyika kwa uchunguzi kuhusu matumizi ya utanzia katika riwaya, kunawanyima wasomaji na wahakiki wa kazi za fasihi kuuelewa utanzia ulimo katika riwaya pendwa kwa kiwango cha juu. Hivyo, utafiti huu ulilenga katika riwaya pendwa za Kiwsahili kwa kuwa mbinu hiyo ya utanzia inaonekana kuwa na athari kubwa katika utanzu husika.

### 1. 3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu umejengwa na lengo kuu na malengo mahususi kama ifuatavyo;

### 1. 3. 1 Lengo kuu

Kuchunguza matumizi ya utanzia katika riwaya pendwa za waandishi teule.

### 1. 3. 2 Malengo Mahususi

a) Kubainisha vipengele vya utanzia katika riwaya za waandishi teule;

b) Kuchambua matukio ya kitanzia katika riwaya za waandishi teule na;

c) Kulinganisha na kulinganua utanzia uliomo katika riwaya pendwa za waandishi teule;

### 1. 4 Maswali ya Utafiti

a) Vipengele vya utanzia katika riwaya za waandishi teule ni vipi?

b) Matukio ya kitanzia katika riwaya pendwa za waandishi teule ni yepi?

c) Kwa namna gani utanzia uliomo katika riwaya za waandishi teule hulandana na kutofautiana?

### 1. 5 Manufaa wa Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yameleta umuhimu ufuatao: Mosi, kusaidia kufahamu tofauti ya tanzia na utanzia. Pili, kuleta manufaa kwa kujua aina za utanzia zilizotumiwa na waandishi teule. Tatu, kuwasaidia watunzi na wasomaji wa kazi za kifasihi kufahamu matumizi ya utanzia katika kazi mbalimbali za fasihi. Nne, kuongezeka kwa kanzi ya tahakiki za bunilizi pendwa za Kiswahili.

### 1.6 Taarifa Fupi za Waandishi Teule

Hapa tutaangazia taarifa fupi ya Ben Mtobwa na Hussein Tuwa ambao ni waandishi teule wa riwaya pendwa katika tasnifu hii.

#### 1. 6. 1 Taarifa Fupi ya Ben Mtobwa

Ben Rashidi Mtobwa alizaliwa tarehe 28/08/1958, katika mkoa wa Kigoma magharibi mwa Tanzania, alisoma shule ya msingi Mgambo, alikuwa na mke anayejulikana kwa jina la Rehema Johnson na walibahatika kupata watoto kumi na wawili. Ben Mtobwa amefariki 9/11/2008. Maisha ya Ben Mtobwa hayakutengana na maendeleo ya uandishi na uchapishaji wa kazi fasihi ya Kiswahili hapa nchini. Ameibukia kuwa miongoni mwa wadau katika nyanja zote za uchapishaji na uandishi. Mtobwa alianza kuandika tangu yuko shule ya sekondari, baadaye alianza kuandika hadithi fupi zilizokuwa zikitolewa katika majarida ya Nchi Yetu, Bara la Afrika na Kiongozi pia, alikuwa akiandika makala katika magazeti ya *Uhuru* na *Mfanyakazi*. Mwandishi Mtobwa alianza kujulikana katika miaka ya (1980) na yuko katika orodha ya waanzilishi na waandishi wa riwaya pendwa za Kiswahili.

Vitabu vyake maarufu ni vile vya muendelezo vinavyomtumia mhusika mkuu Joram Kiango kuwa ni mpelelezi mwenye mbinu kali na uwezo mkubwa katika kazi ya upelelezi. Hadi anafariki dunia tarehe 9/11/2008 alikuwa ameshaandika zaidi ya

vitabu vya riwaya ishirini zikiwaemo hadithi za watoto, riwaya pendwa zenye maudhui ya kipelelezi na riwaya dhati zinazozungumzia mambo mengi yanayoizunguka jamii kama vile: maisha magumu, njaa na siasa. Baada ya kuhangaika sana kutaka kuchapisha kitabu chake cha kwanza ambacho alikiandika akiusawiri wasifu wa aliyekuwa mwanamuziki maarufu nchini Tanzania Remi Ongala, Mtobwa aliamua kukigharamia mwenyewe hadi kikafanikiwa kuchapishwa. Mafanikio yaliyotokana na kitabu hicho yalimpa moyo wa kuendelea kuandika riwaya nyingi ambazo baadhi zilichapishwa na kampuni ya *Series Pacetters* na kampuni zingine kubwa za uchapishaji. Riwaya nyingi alifanikiwa kuzitafsiri kwa lugha ya Kiingereza, na baadhi ya vitabu vyake viliigizwa kama filamu.

Mara baada ya kuanza kupata umaarufu katika masuala ya uandishi mwishoni mwa miaka ya 1980, akawa mkurugenzi mtendaji wa kampuni ya uchapishaji ya Heko Publishers pia, mhariri wa gazeti la kila wiki na Jarida la Heko.

Miongoni mwa riwaya alizoandika ni, *Zawadi ya Ushindi* (1981), *Pesa zako zinanuka* (1984) ambacho pia kilitafsiriwa kwa Kiingereza *Give me money* (1988), *Dimbwi la Damu* (1985), pia kwa Kiingereza kinapatikana kama *A Pool of Blood*, *Najisikia Kuua tena* (1987), *Joram Kiango Mikononi mwa Nunda* (1986), *Tutarudi na Roho Zetu?* (1987), *pia* kilitafsiriwa kwa Kiingereza kama *Zero Hour (*1989), *Salamu Kutoka Kuzimu* (1987), *Roho ya Paka (*1988), *Malaika wa Shetani* (1988), *Dar es Salaam Usiku* (1990), nacho pia kilitafsiriwa kwa Kiingereza kama *Dar es Salaam by Night.* Riwaya nyingine ni *Lazima Ufe Joram* (1983), *Nyuma ya Pazia* (1995), *Kipofu mwenye Miwani Myeusi* (1998), *Mhariri Msalabani* (2000), na *Mtambo wa Mauti* (2004). Pia ameandika hadithi za watoto kama vile *Kisa cha Paka Kupenda Jikoni* na *Mwalimu mwenye Kibyongo.* Aliandika kitabu kinachoitwa

*Kikwete: Safari ya Ikulu* (2005). Pia kuna muswada wa riwaya inayoitwa *Kiguu na Njia* ambao bado haujachapishwa.

IJapokuwa kwa ujumla anaonekana anatumia motifu ya upelelezi akimtumia mhusika mkuu Joram Kiango, baadhi ya riwaya zake zinaonekana kutomtumia mhusika huyo na kujikita zaidi katika mambo ya kijamii. Hata hivyo, wasomaji wengi hutofautisha riwaya zake zingine na kuziita 'Riwaya dhati', miongoni mwa riwaya hizo ni *Zawadi ya Ushindi* iliyobuniwa kutokana na vita vya Uganda na Tanzania. Hali kadhalika, *Dar es salaam Usiku*, ambayo inasawiri maisha magumu yanayosababisha watu kufanya biashara ya kujiuza na *Pesa zako Zinanuka* ambayo imejikita zaidi katika rushwa na mapenzi (Gromov, 2008).

### 1. 6. 2 Taarifa Fupi ya Hussein Tuwa

Hussein Tuwa amezaliwa mwaka 1970, jijini Dar es Salaam, wilaya ya Ilala, kata ya Mchikichini. Ni mtoto wa kwanza katika watoto watatu wa tumbo moja na kuna ndugu ambao amechangia mama na wengine wamechangia baba, jumla wapo wanane. Baba yake bwana Issa Tuwa ni msafirishaji bidhaa nje ya nchi, na mama yake Sango Kipozi ni mtangazaji na mwanahabari mstaafu. Hussein Tuwa alisoma katika shule ya msingi Oysterbay, alipata elimu ya sekondari katika shule ya Masjid Qubah Islamic Seminary, kidato cha tano na cha sita katika shule ya Al-Haramain Islamic Seminary. Shahada yake ya kwanza ambayo ni ya utawala na uongozi (Bachelor of Art-Public Administration) aliipata katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Shahada ya pili ya uongozi wa makampuni (MBA-Corporate Management) Chuo Kikuu cha Mzumbe. Hussein Tuwa ameoa na ana mtoto mmoja.

Hussein Tuwa, kwa hakika alikuwa na ari ya uandishi tangu akiwa sekondari, baada ya kusoma vitabu kadhaa vya waandishi wa hapa nchini kama vile; Musiba, Ganzel,

Mtobwa, Simbambwene na Zahir Zorro; na wa nje ya nchi pia kama Enid Blyton, Agatha Christie, James Hadley Chase, Nick Carter na Rober Ludlum. Lakini alianza hasa kushika kalamu na kuandika riwaya katika mwaka wake wa kwanza akiwa chuo kikuu, pale chuo kilipofungwa kutokana na mgomo na hivyo akajikuta akiwa na muda mwingi mikononi mwake. Ndipo alipoandika riwaya yake ya kwanza iliyoitwa *Mtuhumiwa*, ulikuwa mwaka 1992. Ameshaandika kazi zipatazo 8, nazo ni *Mtuhumiwa, Shangazi kutoka Mjini* (kwa watoto), *Mkimbizi, Utata wa 9/12, Mdunguaji, Bondia, Mtafiti* na *Miss Tanzania*. Miongoni mwa hizi, zilizochapwa ni 5 tu, ambavyo ni *Mkimbizi, Shangazi kutoka Mjini, Mfadhili, Mdunguaji na Utata wa 9/2*. Miegemo ya riwaya zake kimaudhui ni mikasa ya maisha, uhalifu, udhalimu na upelelezi. Hussein Tuwa alishawahi kupata tuzo ya “BURT Award for Afrikan Literature”, kwa kitabu chake kilichoandikwa kwa lugha ya Kiingereza chenye jina la *Temporar Orphan.* Tuzo hii imemuweka miongoni mwa waandishi wa Kitanzania wanaotambulika kimataifa (mazungumzo binafsi). Miegemo ya riwaya zake kimaudhui ni taharuki, mikasa ya kimaisha na kipelelezi. Maudhui yote hasa yanalenga kwenye kuonesha uhalifu na au udhalimu.

Mtafiti alisukumwa na waandishi hawa, kufanya utafiti katika baadhi ya riwaya zao kwa sababu maudhui ya riwaya hizo yamejikita katika utanzia. Pia, majina ya riwaya hizo yamebeba ujumbe mzito unaoibua utanzia kwa jamii. Kwa kuwa mada ya utafiti inahusu utanzia katika riwaya pendwa ya Kiswahili. Hivyo, kuna uhusiano wa wazi na riwaya hizo za waandishi teule.

## 1. 7 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu ulijikita zaidi katika kuchunguza riwaya pendwa nne za Kiswahili, yaani *Dimwi la Damu* (2004) na *Najisikia Kuua Tena* (2015) zilizoandikwa na Ben

Mtobwa pamoja na *Mkimbizi* (2015), na *Mdunguaji* (2012) zilizoandikwa na Hussein Tuwa, ambazo matukio mbalimbali yanayoibua utanzia yamechambuliwa katika kazi hizo. Aidha, tumechagua riwaya hizi kwa sababu zina matumizi ya wazi ya utanzia yaliyotumiwa na waandishi teule. Pia, hata ubunifu wa majina ya riwaya hizi yanaonesha wazi utumikaji wa mbinu ya utanzia katika kazi teule. Dhana ya utanzia iliangaliwa kwa upana zaidi kupitia makala mbalimbali za uchambuzi, ikihusishwa na kazi za kifasihi. Aidha, tasnifu hii imeipanua dhana hii kadiri inavyojitokeza katika kumbo mbalimbali za fasihi. Kwa kufanya hivyo, tumeepuka kuuegemeza utanzia katika utanzu wa tamthiliya pekee.

### 1. 8 Muhtasari wa Sura ya Kwanza

Sura hii ya kwanza, imeonesha tatizo la utafiti linavyoelezea usawiri wa matukio ya kitanzia katika jamii. Pia, sura imejumuisha vipengele mbalimbali vinavyotoa taarifa muhimu za utafiti. Vipengele hivyo ni pamoja na utangulizi, maana ya istilahi muhimu, usuli wa tatizo, tamko la tatizo la utafiti, malengo na maswali ya utafiti. Aidha, umuhimu wa utafiti umeelezwa na kufafanuliwa pia katika sura hii. Kwa ujumla vipengele hivi vinaonyesha jinsi mtafiti alivyojitayarisha kufanya utafiti.

## SURA YA PILI

## KIUNZI CHA NADHARIA NA MAPITIO YA MAANDIKO

### 2. 1 Utangulizi

Sehemu hii inabainisha kiunzi cha nadharia iliyotumika katika uchambuzi wa data na machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada hii**.** Machapisho hayo yamegawanyika katika makundi mawili; kundi la Kwanza, litahusisha maandiko yanayohusu utanzia na kundi la Pili, litahusisha maandiko yanayohusu riwaya pendwa.

### 2. 2 Kiunzi cha Nadharia ya Utafiti

TUKI (2004) inasema kuwa nadharia ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua na kutekeleza jambo fulani. Kwa ujumla, nadharia ni istilahi inayotumika kurejelea kauli au kaida za jumla zinazotengenezwa kwenye uwazaji fulani. Ni kanuni inayojihusisha na mikabala inayotumiwa katika uchunguzi wa suala fulani.

Utafiti huu ulitumia nadharia ya uhalisia kama muongozo wa kuukabili utafiti wake. Hivyo, ukusanyaji wa data na uchanganuzi ulizingatia msingi wa nadharia hii. Uhalisia ni nadharia ambayo husawiri hali halisi na kuzingatia uyakinifu na uhakika wa maisha. Huangalia matukio jinsi yanavyoakisi maisha ya binadamu katika nyanja zote za kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni katika maisha ya kila siku.

Kulingana na Rene Wellek katika jarida la *Neophilologus*, Xiv (1961: 20), dhana ya uhalisia ilianza kutumika takriban mnamo mwaka wa 1970. Katika mwaka huo, Emmanuel Kant katika chapisho lake lililoitwa *Critique of Judgement* aliitumia istilahi ya udhahania kamilifu kama kinyume cha uhalisia. Kufikia mwaka wa 1978,

wahakiki kama vile Schiller walikuwa wakitumia maneno haya yaani udhanifu na uhalisia kuashiria kinyume chake. Kutokana na historia hii, dhana ya uhalisia imekuja kuhusishwa na mikabala miwili. Kwanza, kutumiwa kama njia ya kutathimini hali. Huu ni uhalisia wa maisha. Pili, kuelezea tapo la kifasihi ambalo huashiria uwezo wa kusawiri au kuelezea hali kwa kuzingatia uyakinifu na uhakika wa maisha. Maana hii ya pili ndiyo iliyotumiwa huko Ufaransa na waandishi kama vile Flaubert katika mwaka wa 1850 kuelezea sanaa inayoonyesha maisha ya binadamu jinsi yalivyo. Na katika utafiti huu maana hiii ya pili ndiyo tuliyoitumia katika kuchunguza uhalisia wa utanzia unaojitokeza katika kazi za waandishi teule wa riwaya pendwa ya Kiswahili.

Snow (1968) anaeleza kuwa nadharia ya uhalisia katika upana wake humaanisha uwakilishi wa uhalisi wa mambo katika fasihi. Nadharia hii ilizuka katika karne ya 19 nchini Ufaransa. Nadharia ya uhalisia iliibuka ili kupinga nadharia ya ulibwende ambayo ndiyo ilikuwa maarufu kipindi hicho. Nadharia ilianza kuonekana katika kazi ya Jorge Luis Borger na kuendelezwa na Honors de Blalzae nchini Ufaransa. Hatimaye nadharia hii ilienea sehemu nyingine ulimwenguni kutokana na kazi za wanafasihi mbalimbali. Nchini Uingereza kwa mfano nadharia hii iliiingizwa na kazi za George Eliot, Charles Dickens, Thomas Hardy wakati nchini marekani iliingizwa na kazi za William Dean Housells (Fried, 1987).

Tapo hili liliwekwa msingi na mwanafalsafa anayejulikana kama Hegel katika kitabu chake kinachojulikana kama *Aesthetik* (ujumi). Alilitumia neno uhalisia kumaanisha kazi ya sanaa iliyo na wahusika ambao matendo yao yanachochewa na hali ya kisaikolojia iliyowazunguka. Hegel aliamini kwamba vitu vyote vinavyopatikana humu ulimwenguni ni picha hafifu ya vitu hivyo kama vinavyodhihirika katika dunia

ya kinjozi (Durey, 1998). Waandishi kama Balzac, Stendhal na Flaubert kama wanavyonukuliwa na Wamitila wanasisitiza maelezo ya 'kikweli' katika kazi zao.

Villanueva (1997) anadai kuwa riwaya ya kiuhalisia lazima ionyeshe picha halisi ya maendeleo na matukio ya kawaida ya kijamii. Anaendelea kueleza kuwa thamani ya riwaya ipo katika kuonyesha kwa usahihi migongano ya kijamii pamoja na kueleza hali halisi ya jamii katika kipindi cha historia. Hivyo waandishi wa riwaya hawana budi wa kusawiri ukweli ulioko kwenye jamii na kuonyesha wazi kila dosari kwa lengo la kuleya mabadiliko katika jamii. Dai hili linafafanua kuwa fasihi lazima ionyeshe uhalisia wa kile kinachoendelea katika jamii.

Tallis (1998) anadai kuwa, uhalisia husisitiza uwasilishaji wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa. Mtazamo huu unatia mkazo kwenye uwasilishaji wa mambo ambayo yanaonekana katika jamii. Waandishi wanaodai katika mkondo huu wanatarajia kutoa picha za wahusika, matukio, mandhari ambayo yanaoana kwa kiasi kikubwa na uhalisia wa jamii ya mwandishi anayehusika. Wazo la msingi kwa wana uhalisia ni kwamba wao wanaamii katika matokeo ya mambo na ukweli anaozingatia ni ule unaoweza kuonekana na kuthibitishwa kwa tajiriba. Hivyo basi uhalisia hujikita katika mambo yaliyopo, tukio mahsusi na matokeo yanaweza kuthibitika (Ntarangwi, 2004). Kwa hiyo nadharia hii itasaidia katika kuchunguza matumizi ya utanzia katika riwaya pendwa ya Kiswahili kutokana na malengo yaliyobainishwa.

Wamitila (2002) anadai kuwa kwa kiasi kikubwa tunaweza kusema kuwa kila kizazi huwa na uhalisi wake. Ni katika muktadha huu ambapo tunaweza kuelewa muelekeo wa siku hizi kuhusiana na uhalisia. Katika siku za hivi karibuni, pamezuka aina ya uhalisia ambao unahusisha maajabu. Uhalisiaajabu uaopingana na uhalisia wa

zamani ambao tunaweza kuuita uhalisia wa kirasimi au uhalisia wa kirasimu. Aina hii mpya inajulikana kama uhalisiaajabu.

Waandishi wanaohusishwa na mkondo huu katika hatua za mwanzo ni wa Marekani ya Kusini. Hawa ni waandishi kama Gabriel Garcia Matquez wa Colombia. Juan Rulfo na Carlos Fuentes wa Mexico, Isabel Allende wa Peru, Alego Carpentier wa Cuba, Miguel Asturias wa Guatemala na wengine. Waandishi wa riwaya ya Kiswahili wanaohusishwa na mkondo huu ni S.A.Mohamed, K.W. Wamitila, K. Mkangi, E. Kezilahabi na wengine uhalisiaajabu unatumika katika kazi zao kwa kuchanganya sifa za kiuhalisia na mazingaombwe kama mbinu ya kifani huku wakikusudia kueleza maudhui mazito. Aidha kazi hizi zinavunja muundo wa kikawaida wa utanzu kama njia ya kuzuka na istihara ya miundo ya mifumo ya sasa ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni ya kiulimwengu chini ya mwavuli wa utandawazi.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002) msingi mkuu wa nadharia ya uhalisia ni "usimulizi wa kimuhakati". Huu ni usimulizi ambao unasimulia matukio kama yanavyotokea katika ulimwengu halisi au kwa namna inavyokaribiana sana na ulimwengu hali iliyopo katika jamii. Msingi huu unasisitiza uwasilishaji wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa. Nadharia hii inatia mkazo kwenye uwasilishaji wa mambo ambayo yanaonekana katika jamii.

Uchunguzi wa utanzu wa riwaya unaambatana na uhalisia kwa kiasi kikubwa, hivyo haiwezekani kuizungumzia riwaya bila ya kuyarejelea mawazo yanayohusishwa na uhalisia. Wanauhalisia hufanya hili kwa kujifunga kwenye wahusika wa kawaida au wanaoweza kupatikana katika jamii halisi, kuyachunguza na kuyasimulia maisha yao na tajriba zao, na kusawiri na kuonyesha mandhari na mazingira ya kawaida. Kigezo

muhimu katika uwasilishaji huu wa maisha katika kazi za kihalisia ni dhana ya "Ushabihikweli". Msisitizo mkubwa upo kwenye juhudi za kuukaribia ukweli uliopo katika jamii inayohusika. Dai hili linaendana na maelezo ya Madumulla (2009) ambaye anaeleza kuwa riwaya ni utanzu ulio karibu sana na uhalisia kwa maana kwamba, masimulizi yake yanaendana sana na maisha ya kila siku. Hii inatokana na umakinifu wa utanzu huu katika kudadisi matukio katika maisha. Riwaya haielezi mambo kwa jumlajumla bali inatazama mtu katika ubinafsi wake, akihusianisha na mazingira yake. Uhalisia huu hauonekani katika majina ya wahusika tu, bali hata katika kusema, kula na kuvaa kwake, huku akichochea na maendeleo na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Ntarangwi (2004) anaendelea kudai kuwa imani ya mwanauhalisi ni kwamba kazi ya fasihi yapaswa kuwaweka wanajamii husika katika ulimwengu wao wa kawaida, halisi na wa kweli. Hivyo basi, hata picha za ulimwengu atakazoziumba msanii zinapaswa kudhihirisha uhalisia. Kama ilivyoelezwa hapo awali uhalisia ulikuja kupinga tapo la ulimbwende ambalo lilijikita katika kueeleza mambo kihisia na hakukuwa na uhalisia katika kueleza maisha ya wanajamii.

Hivyo, nadharia ya uhalisia ilitumika kuchunguza matukio ya kiutanzia katika kazi za Ben Mtobwa na Hussein Tuwa kwa kuzingatia hatua zifuatazo; Kwanza, kusoma kazi za waandishi teule na kuhusianisha matukio na mambo mbalimbali ambayo aliyowahi kuyapitia mtafiti maishani. Pili, kuhusisha miktadha mbalimbali iliyomo katika kazi teule na miktadha inayohusisha mifumo ya kiuchumi, kisiasa, na kijamii. Tatu, kutoa maoni yanayoendana na kujazia mapengo kadhaa yaliyomo katika kazi hizo. Nadharia hii ilifaa katika uchambuzi wa utafiti huu kwa sababu, msingi wake mkubwa umejikita katika kuchunguza utokeaji wa matukio ambayo huendana na hali

halisi ya ulimwengu. Hivyo ni dhahiri kwamba matumizi ya nadharia hii katika utafiti huu yamesaidia katika kuelezea uhalisia wa utanzia uliojitokeza katika kazi za waandishi teule wa riwaya pendwa ya Kiswahili kuhusiana na matukio mbalimbali.

## 2. 3 Mapitio ya Maandiko

Machapisho yamegawanyika katika makundi mawili; kundi la kwanza, litahusisha maandiko yanayohusu utanzia na kundi la pili, litahusisha maandiko yanayohusu riwaya pendwa.

### 2. 3. 1 Maandiko Yanayohusu Utanzia

Sengo (1992) anasema kuwa Mazishi ni taasisi ya kuwarejesha waja walikotoka, ama na kuwakumbusha walio hai juu ya marejeo hayo kwa Mola wao. Msiba wa kufiliwa huwa ni faradhi-kifaya kwa Waislamu wote wa ujiranini. Huzuni za kufiliwa huwa ni za wote na kazi kubwa ya majirani na marafiki ni kuwafariji wanandugu waliofiwa. Kazi zote, tangu utoaji wa habari za kifo, uchimbaji ufuo, uoshaji, uchimbaji kaburi, kupatikana kwa tusi, uchukuaji wa jeneza, uzikaji na sala zote za kumsalia maiti ni za jumuiya. Watu wote jumuiani lazima wahusike kwa namna moja au nyingine. Huzuni ya kifo, kwa msingi huchukua siku arobaini. Baada ya hapo hufuata ada ndogo ndogo za dua na kufyagilia mavani kila mara na kila mwaka, daima. Ufafanuzi wa mtaalamu huyu umetubainishia kuwa ndani ya vifo tunaweza kupata matukio yanayofungamana na mazishi ambayo huweza kutoa hisia fulani na kusababisha huzuni na masikitiko.

Saluhaya na Suleiman (2012) wanasema kuwa katika baadhi ya makabila, watani na wajukuu hupaswa kufanya maigizo yanayohusiana na maisha na matendo na tabia ya marehemu. Maigizo haya kama mchezo wa kuigizwa na kusaidia kuwapunguzia

wafiwa huzuni yao, mbali na kutoa mafunzo kwa watu na waliopo msibani. kwa mfano kama marehemu alikuwa na tabia mbaya, basi maigizo haya huipiga vita tabia hiyo kwa njia ya kejeli na dhihaka. Dondoo hii inatoa mwanga kwa mtafiti kwa kuwepo kwa uhusiano wa fasihi na matumizi ya utanzia katika mazingira ya msibani inayoambatana na huzuni. Mfano nzuri unaotolewa na wataalam hawa ni maigizo yenye kusheheni kejeli na dhihaka kwa lengo la kupunguza makali ya huzuni katika maisha ya jamii. Hata hivyo, hoja hii imetoa nafasi ya kuiona kejeli na dhihaka kuwa ni sehemu ya kujenga huzuni.

Mackeon (1974) anasema kuwa tanzia ni aina ya tamthiliya yenye uzito unaodhihirika kihisia au kifikra. Tanzia huwa na suala, matendo na malengo dhati. Aristotle alikuwa mtu wa kwanza ambaye baada ya kuyatazama maandishi ya tamthiliya za Kigiriki aliandika maana ya tanzia katika kitabu chake cha *Poetics*. Kutokana na uchunguzi wake aliona tanzia kuwa ni tamthiliya yenye huzuni ambayo inagusia hisia za watazamaji kiasi cha kuogopesha na kumwonea huruma mhusika mkuu ambaye hupata janga. Andiko hili linatupa dira kuwa hali ya huzuni kwa mtazamaji au msomaji haipo katika tamthiliya pekee. Bali pia, katika kazi nyingine za fasihi kama vile riwaya, ushairi, na nyinginezo. Hivyo, mtaalamu huyu alimsukuma mtafiti kuchunguza matumizi ya utanzia katika riwaya pendwa za Kiswahili

Wamitila (2002) anasema kuwa tanzia huanzia kwenye hatua ya ufafanuzi au maelezo (*exposition*) ambapo mtazamaji au msomaji anaipata picha ya hali iliyopo, mivutano au migogoro inayoanza na utambuzi wa wahusika wakuu. Sehemu hii hufuatiwa na mkweo wa tendo (*rising action*) lililoanza na ambalo baada ya muda huelekea kwenye hali ya kuwa tata (*complication*) kisha kwenye upeo au kilele.

Baada ya upeo hufuata mgeuko, kisha mshuko wa tendo na hatimaye tukio la kuhuzunisha. Mtaalamu huyu anampa mwanga mtafiti kuwa hali ya huzuni haipo katika matendo pekee bali huanzia kwenye maneno au maelezo. Hivyo, utanzia hupatikana pia katika fasihi simulizi na fasihi andishi.

Mkubwa (2000) anafafanua kuhusu utani katika mazishi na matanga. Anafafanua kuwa kuna utani unaofanywa na jamii ya Wapemba kwa kuonyesha tabia zilizofanywa na marehemu. Anaendelea kufafanua kuwa lengo lake ni kupunguza huzuni zilizopo kwa wafiwa. Maelezo haya yametubainishia kuwa maigizo huambatana na utani ili kuwafanya hadhira iwe na furaha wakati linapotokea jambo la kuhuzunisha. Hivyo, hoja hii imemsukuma mtafiti kwa sababu imehusisha fasihi simulizi na hisia za kuhuzunisha ambazo ndio suala linaloshughulikiwa na tasnifu hii.

### 2. 3. 2 Maandiko kuhusu Riwaya Pendwa

Madumulla (2009) anaeleza kuwa, riwaya pendwa pamoja na kuanzishwa miaka ya hamsini hapa Tanzania, ilikuja kustawi miaka ya themanini. Hata hivyo, ilikuwa na matatizo ya kiistilahi, kihistoria, kifafanuzi na kimawanda. Anaendelea kuelezea kuwa riwaya pendwa ya Kiswahili ina sifa ya kuiga mawazo na wakati mwingine hata vitendo kutoka kwenye fasihi pendwa za nchi zilizoendelea. Tena ina upangaji wa haraka wa mtiririko, pia mjadala mkubwa ulikuwepo kwamba, riwaya hii inaangukia wapi kati ya dhati na usahihi ama uchapwa. Matatizo ya kiistilahi ni pamoja na kuitwa majina kama vile, riwaya ya mitaani, riwaya maarufu, riwaya ya taharuki, riwaya pendwa na riwaya ya vijana. Hatimaye, riwaya pendwa ndilo jina lililokubalika. Kazi hii ilimsaidia mtafiti kufahamu matatizo ya kiistilahi katika

riwaya pendwa. Kuonyesha kuwa imetokana na majina tofauti kutokana na upya wake katika uga fasihi.

Mabala (1989) anaeleza athari za riwaya pendwa kuwa ni mwingiliano wa mawazo ya kimaendeleo ya tabaka tawala, umeleta aina ya utamaduni wenye utata katika jamii. Ambapo riwaya pendwa zimeuhakisi mchanganyiko huo, katika wahusika na mandhari. Anaendelea kueleza kuwa falsafa za waandishi wa riwaya pendwa kwa kiasi kikubwa zinaelezea amali za kibepari na za kijamaa ambazo zimewaathiri wakazi wa mjini kwa Tanzania nzima. Andiko hili lilionesha athari za riwaya pendwa bila kuelezea mbinu ya utanzia inavyojitokeza katika kazi ya riwaya pendwa. Hivyo, mtafiti alichunguza matumizi ya utanzia katika riwaya pendwa ya Kiswahili.

Mulokozi (1996) anaeleza kuwa riwaya pendwa ni riwaya ambayo shabaha yake kuu ni kumstarehesha na kumburudisha msomaji. Lengo hili hutimizwa kwa kusawiri visa na vituko vya kusisimua damu, mathalani vituko vya ujambazi na uhalifu, ujasusi na mahaba ya waziwazi. Huweza kuwa na mafunzo kidogo kama lengo la ziada. Mulokozi anaendelea kueleza maendeleo ya riwaya pendwa kulingana na sehemu mbalimbali. Mkondo wa riwaya pendwa ulianzia huko Marekani mwaka 1941, ilipochapishwa hadithi ya Edga Allan Poe ya *The murders in the Rue Morgue.* Baadae mtunzi wa kiingereza Sir Arthur Conan Doyle (1859 – 1930), aliikomaza fani hii na kuifanya ipendwe na kuenea duniani kote. Kazi hii inaonesha kuwa riwaya pendwa ina kazi ya kuburudisha na kustarehesha tu; jambo ambalo si kweli, kwani, inaweza pia kuhuzunisha na kumsononesha msomaji.

Khamisi (2007) akitoa sifa ya riwaya pendwa anaeleza kuwa, riwaya mpya ya Kiswahili ina sifa ya kimaudhui ya kutazama na kuyaona matatizo yetu kwa

msisitizo wa ndani zaidi kuliko nje. Nje inachukuliwa kuwa ni pembejeo tu la matatizo yote. Wakati mwingine, baadhi ya watunzi wa riwaya hii hujitoa kwa kiasi fulani katika kushughulikia matatizo ya ndani ya nchi na kutazama matatizo ya kidunia na kimataifa. Pengine haya yalishughulikiwa kwa kiasi fulani na wanariwaya wa Kiswahili hapo zamani, lakini si kwa msisitizo na vuguvugu hili la sasa. Andiko hili lilimsaidia msomaji kujua kuwa, katika riwaya pendwa kuna matatizo mbalimbali yanayozungunziwa kwa msisitizo yakiwemo ya ndani ya nchi na nje ya nchi. Matatizo ambayo huibua utanzia kwa jamii husika.

## 2. 4 Mapengo Yaliyojitokeza

Kazi za wataalamu hao zimechambua mambo mbalimbali juu ya tanzia na riwaya pendwa kutokana na mitazamo yao. Lakini bado kuna mapengo yaliyojitokeza wazi kama ifuatavyo: Mosi, kuna mkanganyiko wa dhana nzima ya tanzia na utanzia. Pili, hawakuonesha utokeaji wa utanzia katika riwaya pendwa za Kiswahili. Tatu, riwaya pendwa zilizochunguzwa na wahakiki hawakuchunguza matumizi ya utanzia, ambayo yametawala sana katika riwaya hizo. Hivyo, utafiti huu ulilenga kuchunguza matumizi ya utanzia katika riwaya pendwa ya Kiswahili.

## 2. 5 Muhtasari wa Sura ya Pili

Sura hii imeelezea kiunzi cha nadharia iliyotumika katika utafiti huu pamoja na mapitio mbalimbali yaliyotumika. Mapitio yalihusu maandiko mbalimbali ya utanzia na riwaya pendwa za Kiswahili. Maandiko hayo yamezungumzia kwa mapana matumizi ya utanzia yanavyotumika kwa kiasi kikubwa katika fasihi ya Kiswahili.

# SURA YA TATU

# METHODOLOJIA YA UTAFITI

## 3. 1 Utangulizi

Sehemu hii inafafanua mpango wa jumla wa utafiti, eneo la utafiti, jamii ya watafitiwa, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na vikwazo vya utafiti.

## 3. 2 Mpango wa Utafiti

Utafiti huu ulifanyika maktabani na uwandani. Mwelekeo wa utafiti huu ni wa maelezo, hivyo, haukuhusisha kabisa taarifa za kitakwimu. Ukusanyaji, uchanganuzi wa data, pamoja na utoaji wa matokeo ya utafiti huu uliegemezwa katika maelezo. Sehemu kubwa ya data za utafiti huu zilikuwa ni za kimaktaba. Hizi zilikusanywa kwa kutumia njia ya udurusu kutoka katika maandiko mbalimbali yahusuyo utanzia na riwaya pendwa. Data za uwandani zilipatikana kupitia usaili. Usaili kutoka kwa wanataaluma na waandishi watafitiwa.

## 3. 3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu kwa kiasi kikubwa ni wa kimaktaba, ulifanyika katika mikoa ya Dar es salaam na Dodoma. Maeneo hayo yalichaguliwa kutokana na kuwepo kwa vyuo vikuu vyenye maktaba na makavazi yanayolengwa kutumiwa kwa ajili ya udurusu. Vyuo vikuu hivyo ni Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hivi vilisaidia upatikanaji wa vyanzo mbalimbali kama vile ripoti za tasnifu, makala na vitabu.

### 3. 4 Walengwa wa Utafiti

Walengwa wa utafiti huu wamegawanywa katika makundi mawili ambayo ni jamii tafitiwa katika ujumla wake na sampuli iliyoshughulikiwa.

#### 3. 4. 1 Jamii ya Wafitiwa

Taarifa za utafiti zilitarajiwa kupatikana kutoka katika makundi yafuatayo:-

a) Riwaya pendwa mbalimbali zilizoandikwa na Ben Mtobwa na Hussein Tuwa. Hizi zilisaidia kubainisha matukio mbalimbali ya utanzia.

b) Wanataaluma mbalimbali waliozisoma au kuzihakiki riwaya pendwa za Ben Mtobwa na Hussein Tuwa. Hawa walitoa taarifa za utumiwaji wa utanzia.

c) Mwandishi Hussein Tuwa. Alieleza utokeaji wa matumizi ya utanzia katika riwaya pendwa; na

d) Watu kutoka katika familia ya Ben Mtobwa walitoa taarifa za utumiaji wa utanzia katika jamii ya watanzania.

#### 3. 4. 2 Sampuli ya Watafitiwa na Upatikanaji Wake

Sampuli ilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Wawakilishi hao walichaguliwa kulingana na jinsi wanavyokidhi haja na malengo ya utafiti huu.

a) Riwaya mbili kwa kila mwandishi teule wa utafiti huu. Kwa upande wa Ben Mtobwa, ilitumika riwaya ya *Dimbwi la Damu* pamoja na *Najisikia Kuua Tena* na Hussein Tuwa riwaya ya *Mkimbizi* pamoja na *Mdunguaji*. Sifa zilizosababisha kazi hizi zichaguliwe katika utafiti huu ni kuwa na utanzia unaojidhihirika katika namna tofauti.

b) Wataalamu 5 waliozisoma au kuzihakiki kazi mbalimbali za Ben Mtobwa na Hussein Tuwa

c) Mwandishi Hussein Tuwa

d) Watu 5 kutoka katika familia ya Ben Mtobwa.

### 3. 5 Ukusanyaji wa Data

Sehemu hii inaelezea njia na zana mbalimbali zitakazotumika kukusanyia data, pamoja na mchakato wa kukusanya data.

### 3. 5. 1 Njia na Zana za Kukusanyia Data

Njia kuu zilizotumika kukusanyia data za utafiti huu ni udurusu katika maktaba pamoja na usaili uliofanyika uwandani. Zana zilizotumika katika utafiti huu ni muongozo wa usaili na muongozo wa udurusu wa kimaktaba. Zana nyinginezo zilizotumika ni vitabu, majalada, vijidaftari, kalamu, kamera ya picha za mgando na kinasa sauti.

### 3. 5. 2 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data na Udhibiti wake

Mtafiti aliomba ridhaa ya watu binafsi ya watafitiwa. Data za maktabani zilikusanywa kwa njia ya kudurusu, ambapo mwongozo wa udurusu ulitumiwa. Hivyo, mwongozo huo ulitumika katika kusoma tasnifu, vitabu na majalada mbalimbali yanayohusiana na utafiti. Data za uwandani zilikusanywa kwa njia ya usaili.

Mbinu ya usaili ilitumiwa kwa kumuhoji mwandishi Hessein Tuwa, watu 5 kutoka katika familia ya Ben Mtobwa, wataaluma 5 waliosoma au kuzihakiki kazi za Ben Mtobwa pamoja na Hussein Tuwa. Daftari na kalamu vilitumika kunukuu data zilizopatikana katika mahojiano na wakati wa kudurusu kwa ajili ya kutumika wakati wa uchambuzi wa data. Aidha, kinasa sauti na kamera vilitumika kuwarekodia wasailiwa na kupiga picha na vyanzo mbalimbali vinavyohusiana na utafiti huu.

## 3. 6 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data za utafiti huu ulizingatia misingi ya nadharia ya uhalisia. Data zilichanganuliwa kulingana na malengo ya utafiti huu. Hivyo, kila lengo liliunda mada ambayo kila moja ilikuwa na maudhui yanayolandana na mada hiyo. Mbinu ya ufafanuzi ndio ilikayotumika katika kuchambua data katika utafiti huu, mbinu ya kitakwimu haikutumika kwa sababu utafiti huu kwa kiasi kikubwa ni wa kimaelezo. Data zilizopatikana uwandani kupitia njia ya mahojiano zilichanganywa na kuoanishwa na zile zilizopatikana kutokana na udurusu wa kimaktaba kisha kupimwa na kutathminiwa.

## 3. 7 Itikeli za Utafiti

Utafiti huu ulizingatia maadili yaongozayo mchakato wa utafiti. Masuala kama vile uombaji wa barua ya ruhusa kutoka idara husika ya Chuo Kikuu cha Dodoma, kuomba ridhaa ya watafitiwa, utunzaji wa siri za taarifa, na ufichwaji wa majina ya watoa taarifa kadri ya matakwa ya watafitiwa yalizingatiwa.

## 3. 8 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti

Uhalali wa utafiti maana yake ni hali ya utafiti kuwa na uwezo wa kupima jambo au mambo yaliyotakiwa kupimwa au kutafitiwa tu. Na kuhusu uthabiti wa utafiti, ni hali ya utafiti kuweza kutoa matokeo yanayoendana ikiwa utafiti utafanyika katika wakati mwingine au mahali pengine. Vipengele hivi vina uhusiano wa kimjalizo. Kwamba, ni vigumu kwa utafiti kuwa na matokeo thabiti ikiwa uhalali utakosekana (Ponera, 2010). Uhalali wa matokeo ya utafiti huu ulithibitishwa kwa kutumia mbinu zifuatazo: Mosi, kwa kuweka bayana malengo na mipaka ya utafiti. Pili, kwa kutumia lugha nyepesi na ya moja kwa moja katika zana za kukusanyia data ili

sampuli isipate tabu kuelewa kinachotafitiwa; na hivyo, kutoa majibu yaliyohusiana na malengo ya utafiti.

### 3. 9 Vikwazo vya Utafiti

Kuna matatizo mbalimbali yaliyojitokeza wakati wa mchakato wa ukusanyaji wa data za utafiti huu. Matatizo hayo ni kama vile, kutopatikana kwa urahisi kwa baadhi ya sampuli ya watafitiwa wakiwemo, waataluma wa fasihi, kutokana na wengi wao kubanwa na majukumu waliyokuwa nayo. Jambo ambalo limefanya ukusanyaji wa data kutokamilika kwa wakati uliopangwa. Pia, ugeni wa dhana yenyewe ya utanzia kwa watafitiwa, jambo ambalo lilileta shida katika kulitolea ufafanuzi.

### 3. 10 Muhtasari wa Sura ya Tatu

Kwa ujumla sura hii, imeelezea mbinu mbalimbali zilizotumika katika ukusanyaji wa data ili kujibu maswali ya utafiti. Mbinu hizo ni pamoja na mpango wa jumla wa utafiti, eneo la utafiti, jamii ya watafitiwa, ukusanyaji wa data na uchanganuzi wa data, itekeli ya utafiti, uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti na changamoto.

# SURAYA NNE

## MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

### 4. 1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha na kujadili juu ya matokeo ya utafiti. Imegawanyika katika sehemu nne zinazoakisi maswali yaliyouongoza utafiti huu. Sehemu ya kwanza inajadili aina za utanzia. Sehemu ya pili inabainisha vijenzi vinavyoibua utanzia katika fasihi na jamii kwa ujumla. Sehemu ya tatu inachambua matukio ya kitanzia yaliyomo katika riwaya za waandishi teule. Sehemu ya nne inalinganisha na kulinganua riwaya za waandishi teule.

### 4. 2 Vipengele Vinavyobainisha Utanzia katika Riwaya Teule

Kipengele ni jambo au wazo mojawapo katika mada inayojadiliwa. Hapa tuliangalia vijenzi vya utanzia pia, tutaangalia kwa namna gani vijenzi hivyo vya utanzia vinavyoweza kuibua aina za utanzia.

#### 4. 2. 1 Vijenzi vya Utanzia

Vijenzi vya utanzia ni pamoja na vifungo, magonjwa, taabu za safari, migogoro, ugumu wa maisha, ulemavu, ukatili na ajali. Vijenzi hivi husababisha hali ya maumivu, malalamiko, jitimahi, masononeno, huzuni na masikitiko. Maelezo yafuatayo yanaelezea vijenzi hivyo vya utanzia na kutoa mfano mmoja kutoka katika riwaya teule. Kwa sababu sio kila riwaya teule ina mfano wa kijenzi husika.

##### 4. 2. 1. 1 Vifo

Kifo ni tukio au tendo la kufikia mwisho wa uhai, mauti, au uangamiaji. Kifo huweza kumfikia kiumbe yoyote yule, bila kujali umri, jinsia au uwezo wake kifedha. Tukio

la kufa huacha huzuni kubwa kwa jamii husika na kusababisha hali ya majonzi kwa muda fulani. Hivyo, suala la kufa ni kipengele kinachoibua utanzia kwa jamii. Katika fasihi matukio ya vifo yanaelezewa kwa undani kutokana na kwamba mara nyingi huibua uovu wa watu mbalimbali. Mfano wa tukio la kifo katika riwaya ya *Mdunguaji* mwandishi anamtumia mhusika Shani alipofiwa na mumewe. Mtunzi anasema:

> Yule mwanadada alimkumbatia kwa nguvu na kuachia kwikwi ya kilio cha uchungu. "Pole sana shemeji... Kifo ni kazi ya Mungu". Alimnong'oneza kwa sauti ya chini. Yule mwanadada alimuachia na kutikisa kichwa kwa kuafiki maneno yale huku akitoa miwani usoni mwake na kujipangusa machozi kwa kitambaa alichokuwa nacho mkononi na kuirudisha tena usoni ile miwani (uk. 101).

Hapa mtunzi anaonesha jinsi gani kifo husababisha hali ya huzuni. Shani alikuwa akilia kwa uchungu wa kifo cha mumewe kipenzi. Tukio hili la kifo ni halisi katika maisha ya binabamu ambacho ni kijenzi kikubwa kinachoibua hali ya utanzia kwa jamii. Tallis (1998) anathibitisha hili kwa kusema uhalisia husisitiza uwasilishaji wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa,

#### 4. 2. 1. 2 Vifungo

Kifungo ni adhabu ya mtu kuwekwa jela. Kifungo kinaweza kutokea kama mtu amefanya kosa na kuhukumiwa kwenda jela. Mtu anayekwenda jela anaweza kuwa kweli amefanya kosa au amesingizia au hakutenda kosa kwa kukusudia. Kuna aina mbili za kifungo ambazo ni kifungo cha ndani ya gereza na kifungo cha nje. Kifungo cha ndani ni kile anachohukumiwa mtu kwenda jela yaani anakuwa ndani ya gereza. Kifungo cha nje ni kile anachohukumiwa mtu kuishi nje ya gereza lakini anafuata masharti yote yaliyotolewa na mahakama yakiwemo kutofanya kosa tena au kutotoka nje ya wilaya, mkoa au nchi yako. Kipengele hiki kinahusiana na utanzia kutokana na kwamba kinaleta hali ya huzuni na masononeko kwa jamii na mtuhumiwa. Hivyo

hivyo, katika kazi za fasihi. Katika riwaya ya *Mdunguaji* mtunzi amemtumia mhusika Baddi katika kuonesha tukio hilo la kifungo linavyoibua utanzia, anasema:

> Alizolewa na kutupwa kwenye gari la wale askari na kupelekwa moja kwa moja hadi kwenye gereza lililokuwa nje ya jiji la Monrovia ambako alijikuta akitumikia kifungo bila ya hukumu kwa muda wa mwaka mzima. Baddi Gobbos alikata tamaa kabisa ya kuonana tena na yule mwenye mapenzi mazito, na alikata tamaa ya kurudi tena nyumbani kuungana na mke na familia yake (uk. 152).

Nukuu hii inaonesha kwa namna gani kifungo kinavyoweza kuathiri maisha ya mtu kiasi cha kukata tamaa ya kuonana tena na watu wake wa karibu. Baddi Gobbos akiwa ndani ya gereza anajiona mpweke wa kutoiona familia yake na kujikuta akikata tamaa ya kuwaona tena. Tukio kama hili lililomkuta Baddi lipo katika jamii na kuwakumba watu mbalimbali na kuibua utanzia kwa jamii husika

#### 4. 2. 1. 3 Magonjwa

Ugonjwa ni kitu kinachosababisha mtu, mmea au mnyama kuwa katika afya mbaya (TUKI, 2004). Mfano wa magonjwa ni kama vile malaria, UKIMWI, kipindupindu, kifua kikuu, kisukari, saratani, ini, figo, moyo pamoja na magonjwa ya akili. Magonjwa ni jambo halisi linaloleta hali ya utanzia kwa jamii. Kutokana na kuumwa kwa muda mfupi au kwa muda mrefu na kusababisha mgonjwa husika kukata tamaa ya maisha. Pia, ndugu husika hukosa raha na kusimamisha shughuli zao za kimaendeleo na kumshughulikia mgonjwa. Katika riwaya ya *Mkimbizi* mwandishi ameliona hili na kulielezea kwa kumtumia mhusika Kelvin. Anasema:

> Nilipoenda kumuona alikuwa na hali mbaya sana… Siku iliyofuatia hali yake ilibadilika ghafla, na sasa yuko chumba cha wagonjwa mahututi na hawezi hata kuongea, ni ajabu kabisa. Nilipoenda tena kumtembelea, Kelvin alishindwa kabisa kuongea (uk. 139).

Hapa mwandishi anaonesha jinsi ugonjwa unavyoleta hali ya huzuni kwa mgonjwa mwenyewe na kwa jamii yake. Hali ya Kelvin inamtia huzuni shemeji yake

aliyeenda kumuona. Hali kama hii ipo katika jamii, kutokana na kukumbwa na magonjwa kila siku na kusababisha hali ya huzuni kwa jamii husika.

#### 4. 2. 1. 4 Ugumu wa Maisha

Ugumu ni hali ya kutokuwa rahisi kueleweka au kufanyika. Hivyo, ugumu wa maisha ni hali ya kutokuwa rahisi katika kuendesha maisha ya kila siku au upatikanaji wa mahitaji muhimu kama vile malazi, chakula na mavazi. Hali hii husababisha watu kukata tamaa katika maisha na kujawa na huzuni katika maisha yao. Katika fasihi hali hii ya ugumu wa maisha inaandikwa au kusimuliwa na watunzi mbalimbali wa fasihi ili kuenda sambamba na hali halisi ya maisha. Katika riwaya ya *Najisikia Kuua Tena*, mwandishi anasema:

> Ninachotaka kueleza ni taabu niliyoipitia baada ya kumtupa mtoto huyo. Njaa ilinifanya niangukie mikononi mwa mwanamume mwingine. Huyu tangu awali nilijua ananilaghai, lakini sikuwa na njia ya kumzuia asinitie mimba nyingine. Alipogundua nina mimba aliniepuka, ikabidi niteseke sana kutunza mimba hiyo bila mafanikio. Mwisho niliamua kumeza dawa za kuitoa. Ilitoka kwa taabu, na niliponea chupuchupu (uk. 7).

Hapa mtunzi anaonesha kwa namna gani ugumu wa maisha husababisha utanzia. Kitendo cha Machozi kushinda na njaa na kuteseka wakati wa kuitunza mimba aliyokuwa nayo ni cha huzuni na kusikitisha. Hali hii hutokea kwa watu wengi katika katika jamii kwa sababu kuna wengine wanakosa hata pesa ya kununulia maji au dawa.

#### 4. 2. 1. 5 Ulemavu wa Viungo

Ni hali ya kuwa na kiungo cha mwili chenye hitilafu au hali ya kulemaa. katika hali halisi ya jamii, ulemavu na viungo ni kijenzi kimojawapo kinachoibua hali ya utanzia. Ulemavu upo wa aina mbili, aina ya kwanza ni ulemavu wa kuzaliwa kama vile; utasa, chongo, na mengineyo. Aina ya pili ni ulemavu uliosababishwa na kitu au

jambo fulani huu unaweza ni kama vile; magonjwa pamoja na msongo wa mawazo. Hivyo, kusababisha hali ya utanzia katika jamii husika. Kwa hiyo. hata watunzi wa fasihi mbalimbali waliliona hilo ndio maana katika kazi zao wanaandika matukio yanayotokana na kipengele hiki cha ulemavu wa viungo. Katika riwaya ya *Mkimbizi*, mtunzi amemtumia mhusika Wagga katika kusadifu hali halisi ya maisha. Anasema:

> Mtu niliyekuwa nikimtazama sasa hivi alikuwa amepooza sehemu ya kulia ya uso wake na mdomo wake ulikuwa umeanguka upande mmoja na mkono wake wa kulia ulikuwa umejikunja na kubaki ukining'inia kifuani kwake. Mboni ya jicho lake la kulia ilikuwa imeelekea upande mmoja na kukatalia hukohuko (uk. 305).

Nukuu hii inaonesha utanzia wa wazi unaotokana na ulemavu. Kitendo cha kulemaa baadhi ya viungo vya mwili ni cha kuhuzunisha. Hali hii iliyooneshwa na mtunzi ipo katika jamii zetu kwani kuna watu wanapata ulemavu kutokana na sababu mbalimbali katika maisha na kusababisha hali ya utanzia.

**4. 2. 1. 6 Ukatili**

Ukatili ni matumizi ya nguvu yanayompa mtu fursa ya kumtumia au kumkandamiza mtu mwingine ikiwa ni pamoja na kumsababishia kifo, woga au hofu, madhara ya kimwili, kifikra na kisaikolojia (UWAKI, 2013). Ukatili hunaweza kujitokeza kwa kumdhuru mtu kimwili au kumtishia kwa kutumia silaha au kumnyima mtu uhuru wa kufanya uamuzi na kumlazimisha kutenda kinyume na utashi wake. Matukio ya ukatili ni kitendo au mfululizo wa vitendo vya ukatili vinavyofanywa na mtu au kikundi cha watu dhidi ya mtu au kundi la watu kwa makusudi ya kuharibu, kuleta hofu au kutishia amani kwa maslahi binafsi. Vitendo hivyo vya kikatili vinaweza kufanyika nyumbani, kwenye hadhara na mahali popote katika nyakati tofauti. Ukatili umegawanyika katika makundi yafuatayo: ukatili wa wenzi, uhalifu, kimwili, nguvu, mauaji, unatokana na imani za kishirikina, ubakaji na ukatili dhidi ya

wanawake. Kwa mfano, tukio la kikatili katika riwaya ya *Mkimbizi*. Mwandishi anasema:

> Nilikimbia na kumuendea bwana Ubwa Mgaya huku nikiita jina lake bila ya matumaini. Alikuwa ameuawa vibaya sana, kwani bila shaka risasi ilimpata akiwa akijaribu kukimbilia ndani ya hema lake... nilikuwa nikiuona uso wake ukiwa umetokeza kwenye turubai lililotapakaa Damu nyingi sana naye akiwa ametumbua macho (uk. 23).

Hapa mwandishi anaonesha kuwa kwa namna gani ukatili uanavyoibua hali ya utanzia. Kitendo cha Ubwa Mgawa kuuwawa kikatili bila hatia na watu wasiojulikani ni cha kuhuzisha. Tukio kama hili lipo katika jamii kutokana na mtu kuuawa pale anapogundulika anajua siri fulani.

### 4. 2. 1. 7 Ajali

Ni tukio maalum ambalo hutokea katika muda na mahali fulani bila sababu au dhahiri lakini husababisha madhara yaliyo wazi. Ajali huweza kusababisha athari kama vile kupoteza maisha, mali, au kupatwa na ulemavu wa viungo. Kuna aina mbalimbali za ajali zikiwemo ajali ya moto, gari, ndege, meli, bomu, kubomoka au kubomolewa kwa majengo, mafuriko na mengineyo. Katika jamii matukio kama hayo yanaleta utanzia kwa mtu au kikundi cha watu. Kwa mfano, katika riwaya ya *Najisikia Kuua Tena* mtunzi anasema:

> Lingine ni matokeo yaliyotokea pindi tukikuleta hapa. Ulikuwa kwenye gari aina ya Landrover iliyokuwa ikiendeshwa na askari wangu. Msichana wako alikuwa katika hiyo gari pia. Gari hiyo ilipokuwa imalize barabara ya Morogoro iingie mtaa wa Umoja wa Mataifa iligongwa na gari nyingine aina ya Landrover. Wewe kwa kuwa ulikuwa umelazwa kwenye kiti hukudhurika. Dereva wangu ameumia kidogo. Lakini msichana wako… (uk. 103)

Hapa inaonesha kuwa hali ya utanzia unaosababishwa na ajali. Akina Jorom wanapata ajali ya gari wakiwa wanaelekea hospitali. Kitendo hiki kipo katika jamii zetu ambacho husababisha utanzia. Kutokana na kwamba ajali inaweza kutokea

wakati wowote na pahali popote hivyo, jamii kuingia katika wakati mgumu. Villanueva (1997) anathibitisha hili kwa kusema kuwa riwaya ya kiuhalisia lazima ionyeshe picha halisi ya maendeleo na matukio katika jamii.

### 4. 2. 1. 8 Mabaa Makubwa

Baa ni kitu kiletacho hasara, maafa au shida. Mabaa makubwa ni yale matukio ambayo yanaleta hasara kubwa kwa jamii husika. Mfano wa mabaa hayo ni njaa, mafuriko, tsunami, kimbunga, tetemeko la ardhi pamoja na vita. Hali hii husababisha jamii kuingiwa na huzuni kutokana na madhara yanayosababishwa na matukio haya makubwa. Katika fasihi mambo kama haya yanazungunzwa ili kwenda sambamba na matukio halisi yanayoikumba jamii. Kwa mfano, tukio la vita katika riwaya ya *Dimbwi la Damu* linavyoibua hali ya utanzia. Mtunzi anasema:

> Hatukusubiri sana kabla maadui hawajatufikia. Tuliwaacha kuingia vyema katika mtego wetu. Nilipohakikisha kuwa wamezingirwa barabara nilitoa ishara. Kilichofuata ni kitu ambacho hadi leo hii naogopa kukifikiria. Milio ya bunduki na marungu ilivuma ghafla. vilifuata vilio vya watu waliokuwa wakifa, damu ilimwagika mfano wa maji yasiyo ya thamani, uhai wa watu ukiteketea mithili ya nyasi zinazoungua moto (uk. 106).

Hapa mwandishi anaonesha kwa namna gani vita vinavyoweza kuathiri watu kijamii, kisiasa na kiuchumi. Nchi ya Ngoko ina migororo ya kisiasa iliyosababisha kikundi cha CHECHE kuingia msituni kupigana vita kati ya serikali iliyo madarakani na kikundi hicho. Na matokeo yake watu wengi wanapoteza maisha, sio maadui wa cheche tu hata watu wao pia walikufa. Tukio hili la kuhuzunisha katika uwanja wa vita lipo katika maisha halisi yanayosababishwa na migogoro ya kisiasa.

### 4. 2. 2 Aina za Utanzia

Utanzia umetokana na dhana mama ya tanzia, hivyo hata aina za utanzia zinatokana na kuhusianishwa na tanzia. Utafiti umebaini kuwa, aina za utanzia zinatokana na

vijenzi vinvyoibua hali ya utanzia kwa jamii. Zaidi, wazo la kubainisha aina za utanzia kwa kuangalia matukio yanayoibua utanzia yametoka kwa Mutembei (2016)[1] anayesema kuwa utanzia ni hali inayotokana na matukio ya kuhuzunisha na kusikitisha na husababishwa na tukio linalotokea kwa kuigusa jamii. Hivyo, aina za utanzia zipo na zinajitokeza tofautitofauti kulingana na tukio hilo. Kuna matukio mbalimbali kama vile mafuriko, kifo, na kukatwa viungo vya mwili kwa albino.

Hoja hii imetupa mwanga kuwa aina za utanzia haziwezi kutoka hewani bali zinatokana na vijenzi vinavyoibua utanzia huo. Hivyo, kwa kuzingatia mawazo hayo tasnifu hii imebaini kuwa kuna aina tatu za utanzia ambazo ni utanzia wa kisaikolojia, kimwili na kimaumbile. Maelezo yafuatayo yanashadadia aina hizo za utanzia na kutoa mfano mmoja kutoka katika riwaya teule.

#### 4. 2. 2. 1 Utanzia wa Kisaikolojia

Saikolojia ni elimu inayohusiana na ufahamu na utendaji kazi wa nafsi au akili ya binadamu (TUKI, 2004). Kwa mujibu wa tasnifu hii utanzia wa kisaikolojia ni tukio la hasara ya hisia, akili, kijamii na kiroho. Kwa mfano wa hasara ya kisaikolojia ni pamoja na kifo cha ndugu, rafiki au jamaa, usumbufu wa bosi kazini, kufukuzwa kazi, kufungwa jela. Aina hii ya utanzia wa kisaikolojia inasababishwa na hamu ya kitu ambacho hakiwezekani kupatikana. Kutokana na maelezo hayo, inawezekana saikolojia ni nyenzo muhimu katika maisha ya uwerevu na utambuzi wa binadamu. Zaidi, inaweza kuharibiwa inapokumbwa na matukio ya kitanzia kwani utanzia hujumuisha matatizo yanayotokea katika harakati za maisha ya binadamu. Aidha, watunzi wa fasihi wameliona hili na kutunga kazi zinazoendana na utanzia wa

[1] Mahojiano baina ya Prof. Mutembei na mtafiti yaliyofanyika Machi 15, 2016 jijini Dar es Salaam. Prof. Mutembei ni mhadhiri wa fasihi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

kisaikolojia. Mfano wa aina hii ya utanzia tunaipata katika riwaya ya *Mdunguaji*, mtunzi anasema:

> Gilda alitikisa kichwa kwa masikitiko makubwa... kwangu mimi alikuwa ni mtu nzuri sana. Alinirejeshea heshima fulani niliyobaki nayo hapa duniani, alinijali na aliniamini sana. Siku hiyo tulikuwa tumejipumzisha chumbani kwetu pale hotelini ndipo watu wenye magwanda na siliha walipovamia na kuanza kumpiga... "wakamchabanga marisasi mbele ya macho yangu" Alisema huku akiangua kilio... Wakamuua bwana kama mbwa (uk. 140).

Nukuu hii inaonesha kwa namna gani kifo kinavyoweza kusababisha utanzia. Kitendo cha mauaji ya mpenzi wa Gilda kilimuhuzunisha na kumsikitisha kiasi cha kwamba anashindwa kuzuia hisia zake kila anapozungumzia tukio hilo. Hali hii ipo katika jamii pale mtu anapofiwa na mtu wake wa karibu.

#### 4. 2. 2. 2 Utanzia wa Kimwili

TUKI (2010) inasema kuwa mwili ni umbo lolote la mnyama au binadamu kuanzia kichwani hadi miguuni. Yaani, hujumuisha sehemu kama vile kichwa, mikono, masikio, macho, tumbo na miguu. Kwa mujibu wa tasnifu hii, hali ya utokeaji wa utanzia huweza kujitokeza katika viungo mbalimbali vya mwili. Mabadiliko ya kimwili huweza kusababisha ukosefu wa uhuru, utu, na uwezo wa kufanya kazi kutokana na maumivu ya mwili yaliyosababishwa na magonjwa mbalimbali au maumivu yanayotokana na kupigwa pamoja na kuchomwa na kitu kinachosababisha maumivu. Hivyo, imani yetu iliyojengeka ndani ya tasnifu hii ni kuwa mwili ni nyenzo ya msingi katika kukabiliwa na matukio ya kitanzia. Aidha, katika kazi za fasihi watunzi hutumia mwili kuibua matukio ya kitanzia. Katika riwaya ya *Mkimbizi* mwandishi amemtumia mhusika Tigga katika kuonesha kwa namna gani mwili ukipatwa na maumivu husababisha utanzia, anasema:

> "Sasa nikikupa huo mkanda halafu mimi hatima yangu itakuwa nini?" Nilimuuliza kwa kebehi. Alinibamiza kofi kali sana la ghafla na macho yalinichomachoma kwa machozi machanga. Nikiwa sijawahi kupata kipigo cha aina yoyote ile kwa miaka mingi sana, vipigo nilivyopata siku ile viliniuma sana (uk. 76).

Nukuu hii inaonesha jinsi kipigo katika mwili huweza kusababisha hali ya maumivu. Kitendo cha Tigga kupewa kipigo na askari mwanamke kilimuhuzunisha na kumpa maumivu makali. Hali hii ipo katika hali halisi ya maisha katika jamii kutokana na kuwa mwili ukipatwa na maumivu yanayotokana na sababu fulani husababisha hali ya huzuni.

#### 4. 2. 2. 3 Utanzia wa Kimaumbile

Maumbile ni tabia au umbo la asili la kiumbe (TUKI, 2004). Kwa mujibu wa tasnifu hii, ni aina mojawapo ya utanzia ambayo inatokana na ulemavu katika mwili wa binadamu, ulemavu huo ni ule wa kuzaliwa, yaani, wa asili. Kwa mfano, utasa au ugumba, kuzaliwa na chongo, kuzaliwa na upungufu wa kiungo kimoja mwilini, umbilikimo, na ulemavu wa ngozi, katika fasihi waandishi wanatunga kazi zao kwa kutumia ulemavu wa namna hii. Pia, katika jamii ulemavu huu unawapata watu wengi huzuni kusababisha kukata tamaa katika maisha.

Hivyo basi, utanzia wa kimwili ni ule unaotokana na maumivu ya mwili yaliyosababishwa na magonjwa mbalimbali, maumivu yanayotokana na kupigwa, au kuchomwa na kitu kinachosababisha maumivu hayo. Wakati utanzia wa kimaumbile unatokana na kuzaliwa na upungufu wa kiungo fulani katika mwili kama vile ugumba au utasa.

### 4. 3 Utanzia katika Riwaya za Waandishi Teule

Tasnifu hii, imebaini kuwa utanzia ni miongoni mwa mbinu za kibunilizi zinazotumika katika fasihi hususani fasihi pendwa. Hapa tunachambua matukio ya kitanzia yaliyomo katika riwaya pendwa za waandishi teule

#### 4. 3. 1 Riwaya Teule za Ben Mtobwa

Riwaya za Ben Mtobwa zilizotafitiwa ni *Najisikia Kuua Tena* na *Dimbwi la Damu*. Maelezo yafuatayo yanahusu muhtasari wa kazi hizi.

##### 4. 3. 1. 1 Muhtasari wa Riwaya ya *Najisikia Kuua Tena*

Riwaya hii imechapishwa mwaka 2015 chapa ya tatu ikiwa na jumla ya sura 19. Inazungumzia wasaliti wa nchi walio na uchu wa madaraka na kusababisha vifo vya watu mbalimbali wasio na hatia. "Inspekta najisikia kuua tena…" Inadai sauti ya upande wa pili wa simu iliyomo mikononi mwa Inspekta Kombora. Hii ikiwa simu ya pili, baada ya awali ambayo ilifuatiwa na kifo cha mwandishi maarufu wa vitabu, inamtia Inspekta hasira kali, nusu ya wazimu. Anafanya yote yaliyo ndani ya uwezo wake ili kumtia mtuhumiwa mikononi kabla hajaua tena… Hapatikani! Taarifa za vifo hivyo zinavuja na kuvifikia vyombo vya habari. Joram Kiango ni miongoni mwa watu wanaoipokea habari hiyo ya kutisha kwa mshangao. Akisaidiana na mpenzi wake Neema, na polisi wanaongozwa na Ispekta Kombora, anajikuta akipambana na kundi la siri lijiitalo TWAA, ambalo lina nia ya kuivuruga nchi ya Tanzania na hatimaye kutwaa madaraka ili kuizua nchi hiyo isijenge ujamaa na isivisaidie vyama vya wapigania uhuru.

Kundi la TWAA linaanzisha msululu wa mauaji ambayo baadhi yake yamekusudiwa kuzuia siri ya mipango yake ya kuangusha serikali isitoke nje. Anayefanya mauaji

hayo ni kaburu Bon. Kiango na Kombora wanapeleleza mauaji mpaka Kiango anagundua kuwa kuna njama za kimataifa za kisiasa katika suala zima, hasa baada ya kuipata karatasi ya siri yenye kueleza azma ya TWAA. Baada ya mipango yao kugundulika, mahaini wa TWAA wanauwawa katika mapambano na polisi. Hivyo, mpango wao unazimwa. Riwaya ya *Najisikia Kuua Tena* imetumia muundo wa moja kwa moja, ikielezea masuala kama vile usaliti, uzalendo na tamaa. Aidha, mwandishi ametumia mandhari ya jiji la Dar es Salaam.

#### 4. 3. 1. 2 Muhtasari wa Riwaya ya *Dimbwi la Damu*

*Dimbwi la Damu* ni riwaya iliyochapishwa mwaka 2004 chapa ya pili ikiwa na jumla ya sura 7. Riwaya hii inasimulia matukio ya mauaji ya kutisha ambayo yametokea ndani na nje ya Tanzania. Riwaya inaanza kwa kusimulia wapenzi wawili, Maimuna na Juma, wanaokutwa chumbani wamekufa, yamkini kwa kunywa sumu. Mpelelezi mashuhuri Joram Kiango haridhishwi na maelezo ya watu juu ya vifo hivi, anaamua kufanya upelelezi. Upelelezi unamfikisha kwa Bob aliyekuwa mpenzi wa Maimuna. Kabla Kiango hajapata habari anazozitaka, Bob anakufa maji. Inabidi Kiango apeleleze kwa nini na vipi Bob amekufa. Katika kupeleleza kifo hicho, Kiango anagundua kwamba Bob alikuwa na uhusiano na chama kimoja cha siri cha nchi jirani kiitwacho CHECHE ambacho kina nia ya kuiondoa kwa mtutu wa bunduki serikali ya nchi hiyo. Anagundua kuwa, chama hicho kimemteka nyara Balozi mdogo wa nchi yao ili kujitangaza. Inabidi Kiango apambane na chama hicho hadi anapofanikiwa kumtoa Balozi huyo.

Mwishoni, Kiango anakutana ana kwa ana na kiongozi wa wapiganaji wa CHECHE na kupata maelezo kamili kuhusu kifo cha Bob na madhumuni ya chama hicho. Mtiririko wa visa katika riwaya hii si changamani. Riwaya ya *Dimbwi la Damu*

imesimulia masuala ya kisiasa, usaliti, mapenzi na uzalendo. Mandhari aliyotumia mwandishi ni ya Kigoma na nchi jirani.

### 4. 3. 2 Matukio ya Kitanzia katika Riwaya za Ben Mtobwa

Sehemu hii inabainisha matukio yenye kuibua utanzia katika riwaya mbili za mwandishi Ben Mtobwa ambazo ni *Najisikia Kuua Tena* na *Dimbwi la Damu* ambazo zilichunguzwa.

#### 4. 3. 2. 1 Matukio ya Kitanzia katika Riwaya ya *Najisikia Kuua Tena*

Matukio ya kitanzia ni yale yanayoibua hali ya huzuni, masikitiko, masononeko na mateso kwa hadhira au jamii. Hali hii imejitokeza kwa kiasi kikubwa katika riwaya ya *Najisikia Kuua Tena*. Jina lenyewe la riwaya linaonesha utanzia, kitendo cha kujisikia kuua husababisha utanzia kwa jamii. Mwandishi anamtumia msichana Machozi ambaye alipewa mimba na Kitenge. Hata hivyo, Kitenge anamtelekeza msichana huyo na kusababisha kumuweka Machozi katika wakati mgumu. Hatimaye, anajifungua mtoto wa kike; kutokana na hali ngumu ya maisha anaamua kumtupa mtoto huyo kwenye pipa. Anasema:

> Nikikuruhusu kusema utaanza kuikana mimba hiyo. Waweza hata kudai kuwa hujawahi kufanya nami mapenzi ingawa ni wewe uliyeniharibia ubikra. Napenda kukufahamisha kuwa mwanao alikuwa msichana. Nilimtupa katika mapipa ya takataka za hospitali ya Maweni. Kama walimuokota akiwa hai au maiti, sijui. Sikujali. Najua na wewe hujali wala usingejali (uk. 7).

Nukuu hii inaonesha hali ya utanzia kutokana na matukio mawili; Kwanza, kutelekezwa kwa msichana Machozi hali ya kuwa mjamzito. Na pili, kitendo cha Machozi kuamua kumtupa mtoto asiye na hatia. Aidha, mwandishi anatuonyesha jinsi ukatili huo wa wanaume unavyoweza kuleta mateso makubwa kwa wanawake; Kwani, Machozi alijikuta akijiingiza kichwa kichwa kwa wanaume wenye uchu wa mapenzi. Kitendo ambacho kilisababisha Machozi kunasa mimba nyingine na

kuamua kuitoa. Hali hiyo ilisababisha kutaka kupoteza maisha na kujikuta akiangukia kifungo cha miaka mitatu gerezani. Mwandishi anathibitisha hilo anasema:

> Ninachotaka kueleza ni taabu niliyoipitia baada ya kumtupa mtoto huyo. Njaa ilinifanya niangukie mikononi mwa mwanamume mwingine. Huyu tangu awali nilijua ananilaghai, lakini sikuwa na njia ya kumzuia asinitie mimba nyingine. Alipogundua nina mimba aliniepuka, ikabidi niteseke sana kutunza mimba hiyo bila mafanikio. Mwisho niliamua kumeza dawa za kuitoa. Ilitoka kwa taabu, na niliponea chupuchupu (uk. 7).

Kwa hakika, nukuu hii imemchora Machozi kama mwanamke aliyeteseka sana katika maisha yake. Hii inaakisi hali halisi ya jamii nyingi za Kitanzania ambazo wasichana hujikuta katika wakati mgumu baada ya kupachikwa mimba na kukataliwa na muhusika wa mimba hiyo. Kitendo hiki katika jamii huwa kinawatokea sana wasichana hususani wanafunzi ambao wahusika wa mimba wazikataa. Hii inatokea aidha kwa kuogopa kufungwa jela, ugumu wa maisha au kutokana na sababu zao binsfsi.

Mwandishi katika riwaya ya *Najisikia Kuua Tena* ametumia matukio ya mauaji ya kutisha katika kuibua utanzia. Amemtumia mhusika kaburu Ben kama muuaji mkubwa katika riwaya hii. Na kusababisha mauaji mbalimbali yakiwepo ya Kitenge akitumia jina bandia la Bazile. Anasema:

> Ilikuwa usiku wa manane alipokurupuka ghafla kwa maumivu makali ambayo yalipenya kifuani kwake. Mkono wenye nguvu ulimkandamiza asiweze kuinuka kutoka kitandani hapo. Mkono wa pili ulimziba mdomo hata akashindwa kutoa sauti. Pigo la pili lilipenya hadi moyoni, Kitenge akahisi maumivu yakipungua na badala yake akimezwa na usingizi mzito wenye kiza cha kutisha (uk. 18).

Tukio hili linaonesha hali ya maumivu aliyoyapata Kitenge kabla ya kufariki dunia. Mwandishi anaonesha utanzia wa waziwazi, kwani tukio la mauji ya kitenge ni la

kusikitisha na kuhuzunisha. Aidha, mauaji haya ya kusikitisha yanamkuta pia, Wamangi ambaye anauliwa na muuaji yuleyule aliyemuua Kitenge. Mtunzi anasema:

> Nilikuwa nimefungwa kamba mikononi na kitambaa mdomoni. Nikajitahidi hata kamba hizo zikafunguka. Nikarejea chumbani ambako niliyoyakuta yalikuwa hayatazamiki. Mume wangu mpenzi alikuwa kalala chali kitandani, uchi kama alivyolala usiku wa jana, mwili wake mzima ukiwa umeloa damu nzito ambayo ilikuwa ikiendelea kutiririka kutoka katika jeraha baya mno la kisu au sime lilokuwa wazi kifuani. Sikuweza kutazama mara mbili. Nadhani nilianguka na kuzirai (uk. 35).

Hapa mwandishi anaonesha tukio hili la kusikitisha lilivyoleta madhara kwa mke wa marehemu. Hali ambayo ilisababisha kupoteza fahamu kwa muda. Pia, mwandishi anatuonesha tukio lingine la kuhuzunisha la mauaji ya Jugeni. Muuaji anajitokeza kama jitu la ajabu, na lenye nguvu sana ambalo halishindwi na jambo lolote lile. Mtunzi anasema:

> Mara alihisi kuinamiwa na dude refu jeusi na alipojaribu kufumbua macho yalizibwa kwa mkono wenye nguvu kama chuma. Juhudi zake zote za kuutoa mkono huo hazikufua dafu. Alipojaribu kurusha teke lilidakwa kwa mkono mwingine. Dakika hiyohiyo jisu kali lilipenya kifuani kwake kwa maumivu makali. Hakuwahi kupiga kelele, kwani mkono uliokuwa usoni ulihamia mdomoni kuuziba. Pigo la pili lilimmaliza. La tatu hakulisikia kabisa (uk. 36).

Nukuu hii inaonesha kwa namna gani marehemu alipokuwa akijaribu kutetea uhai wake. Hata hivyo, jambo hilo lilishindikana kwa huyu muuaji katili, na hatimaye akapoteza maisha. Hapa ni wazi kuwa muuaji alikuwa na mbinu nyingi katika kutekeleza hila yake. Vitendo hivi vya mauaji kwa watu wasio na hatia vinavyofanya na watu wenye uwezo kifedha au mwenye cheo serikarini vipo katika jamii yetu halisi. Watu hao wanafanya kutokana na kutaka kumiliki mali zaidi, kutunza siri zao ambazo hazifai kwa jamii au kutokana na sababu wanazozijua wao wenyewe.

Mwandishi anaendelea kuonesha hila za muuaji huyu ambaye anaziendeleza hata kwa askari polisi. Ili kutoa onyo kwa serikali, anaamua kumjeruhi vibaya mmoja wa askari polisi. Anaposema:

> Polisi huyo hakuwahi kusikia yote. Alikuwa hajifai kwa kutetemeka, kutetemeka ambako kulikoma na nafsi yake kuchukuliwa na mshtuko mkubwa pindi kisu hicho kilipopita ghafla kifuani na kuacha jeraha kubwa kwa alama ya msalaba. Maumivu hayo makali pamoja na mshtuko vilimfanya aruke na kuanguka sakafuni ambako alitulia kwa dakika nzima kama anayesikiliza ili afahamu kama yungali duniani au tayari kawasili kuzimu (uk. 47).

Hapa mwandishi anaonesha hali ya kusikitisha inavyoendelea kutendeka mpaka kwa walinda amani ya nchi. Kitendo hiki huwapa hofu hata raia juu ya muuaji huyo. Katika jamii yetu matukio kama haya ya vitisho wanayokumbana nayo polisi yapo na yanaendelea kuwepo. Polisi wanakuwa katika wakati mgumu katika harakati za kupambana na waarifu katika jamii husika. Hivyo, kusababisha hali ya huzuni kwa mapolisi hao na jamii kwa ujumla, hii inaonesha kwa namna gani fasihi inavyoshabihikweli katika maisha halisi ya jamii.

Aidha, mtunzi anaendelea kuonesha matukio ya kitanzia katika riwaya hii ya *Najisikia Kuua Tena*. Anamtumia pia mhusika Komba ambaye aliokota nyaraka za siri ya kuipindua nchi na kuzificha,ambapo naye anatakiwa kuuawa. Hata hivyo, Joram Kiango katika harakati za kumsaidia asiuawe anachelewa. Mtunzi anasema:

> "Wameshaniua nakufa…Nakufa…" Komba aliendelea kulalamika.
> "Wewe sio mmojawao?"
> "Mimi ni adui yao mkubwa."
> "Wewe ni nani?"
> "Huwezi kunifahamu. Kwa jina ni Joram Kiango."
> "Joram! Nakujua sana…" Komba alisema kwa juhudi kubwa. "Joram! Walinitesa sana…" Laiti wangeniua… nilikuwa sina hali siku zote. Nikienda huku nakutana nao. Nikikaa hapa usiku wanafika na kuniadhibu kwa vitisho na mateso. Wameniua…" akaanza tena kulalamika (uk. 76).

Nukuu hii inaonesha tukio la mateso analokumbana nalo mhusika Komba. Ingawa alikuwa na nia nzuri tu ya kuikomboa nchi yake isiingie katika machafuko ya kisiasa na hatimaye anapoteza maisha.

Pia, tendo hili la mauaji linatokea kwa raia mwingine asiye na hatia, Bazile, ni raia ambaye jina lake lilitumika katika kufanya mauaji ya kutisha. Ili kuficha ukweli wa mambo wauwaji wanaona bora naye auawe. Anasema:

> "Wapi?" Bazile alihoji kwa udhaifu huku akijikongoja kuinuka. "Fanya haraka!" alifokewa. Kama kondoo aliinuka na kufuata mlango alikoelekezwa. Baada ya kupita milango na vyumba kadhaa, aliamriwa kusimama.
>
> "Geuka huku." Alipogeuka alikutana na risasi ya bastola isiyo na mlio ambayo ilimfanya ausahau udhaifu wake na kupaa juu. Alipotua chini tena alikuwa chali, damu nzito zikimvuja huku akiwa tena kamezwa na aina nyingine ya usingizi ambao haukuwa na ndoto wala hisia (uk. 95)

Hapa mwandishi anaonesha mateso yanavyosababisha utanzia. Hata hivyo, haikutosha, aliamua kummaliza kwa kumpiga risasi. Watu kama hawa akina Komba ambao wapo tayari kufa kwa ajili ya nchi yao wapo katika jamii inayotuzunguka,wana uchungu na nchi yao na kuonesha kitendo cha kizalendo.

#### 4. 3. 2. 2 Matukio ya Kitanzia katika Riwaya ya *Dimbwi la Damu*

Katika riwaya hii, mwandishi ametuonesha pia matukio mbalimbali ya kitanzia. Kama lilivyo jina lenyewe la riwaya *Dimbwi la Damu,* ni wazi kuwa kuna mfululizo wa matukio ya kitanzia.

Tukio la kwanza linamhusisha mhusika Maimuna ambaye anapata maumivu makali kutoka kwa mpenzi wake Bob baada ya kumkuta na mwanamke mwingine. Bob anamtolea maneno ya kejeli Maimuna kiasi kwamba anamuona Maimuna ni kituko mbele ya macho yake. Anasema:

> Maimuna alijikuta kasimama mbele yao akiwatazama kwa mshangao.
> “Bob, nani huyo?” aliropoka baada ya kuushinda mshangao wake.
> “Ni mchumba wangu,” Bob alimjibu kwa sauti ya kijeli.
>
> “Wala sidhani kama una haki ya kuingia hapa bila mwaliko. Naona uende zako haraka kama ulivyofika.”
>
> “Bob, kweli unaniambia mimi maneno hayo? Siyaamini masikio yangu.”
>
> “Amini usiamini, sijali. Nakutaka upotee mara moja.”
>
> “Bob!...”
>
> “Ondoka.” Sasa Bob alifoka kwa nguvu. Sauti yake kali ikamwingia Maimuna hadi moyoni kama mshale wa sumu, sumu ambayo ilimletea maumivu makali. Ndio kwanza ikaonekana kuwa Bob hakumpenda kamwe, bali ulaghai na hongo zake alizotoa ili aitulize tamaa yake tu (uk. 23).

Hapa mwandihi anaonesha hali ya masononeko aliyokuwa nayo Maimuna, kutokana na kukataliwa na mwanaume ambaye aliamini anampenda kwa moyo mmoja. Kumbe alikuwa anajidanganya, Bob hakuwa na mapenzi ya dhati kwa Maimuna. Suala la usaliti katika jamii linajitokeza katika maeneo tofautitofati kama vile; usaliti wa mapenzi, kazi, mali na vingine vinavyofanana na hivyo. Hivyo, kitendo cha kusalitika katika jamii yetu kinaendelea kuwepo na kusababisha watunzi mbalimbali wa fasihi kutunga kazi zao kuendana na ukweli ulipo katika jamii.

Aidha, mhusika Juma anaamua kutoa uhai wake kwa sababu ya kukataliwa na Maimuna. Baada ya Maimuna kwenda kwa Bob, Juma anaitumia nafasi hiyo kujitoa uhai kwa kunywa sumu iliyokuwa ndani ya chupa. Mtunzi anasema:

> Alimkuta Juma katika hali iliyomfanya atetemeke na kutamani kukimbia. Alikuwa kalala chini akigaagaa kwa namna ya maumivu makali. Kando yake kulikuwa na chupa iliyoandikwa asidi ikiwa imejaa nusu…” Sina njia nyingine ila kujiua. Maisha yangu yote yalikuwa na thamani kwa ajili yako. Hivyo, kukukosa sina haja wala sababu ya kuendelea kuishi. Kwa heri, mpenzi” (uk. 24).

Hapa mtunzi anaonesha jinsi gani mapenzi yanaweza kusababisha kifo cha mtu kutokana na kukataliwa. Kitendo ambacho kipo katika jamii ambacho kinamkuta mtu

baada ya kusalitiwa na mpenzi wake ambaye aliamini hawataachana milele na kusababisha hali ya utanzia kwa jamii husika. Mtunzi anaendelea kulionesha hili kwa kumtumia mhusika Maimuna. Anasema:

> Hapa amelala mtu pekee aliyenipenda, mtu pekee ninayempenda, mtu ambaye amekuwa mpenzi wangu mwaminifu tangu utotoni hadi siku ya kufa. Amelala, hataamka tena. Kalala milele, kwa ajili yangu. Tazama anavyotabasamu, tangu alipofahamu kuwa nampenda. Uaminifu ulioje kama na mie nitaamua kulala naye milele! Upendo ulioje kama tutalala pamoja hadi siku ya kiama! Mapenzi yaliyoje… mahaba yaliyoje…" Hakusubiri kuwaza kwa mara ya pili. Bali aliirukia chupa ya sumu iliyobaki nusu na kuimeza yote. Wakati ikianza kufanya kazi yake mwilini akajilaza kando ya mwili wa Juma na kumkumbatia kwa nguvu huku akinong'ona "Juma… Nisubiri tusafiri pamoja… nisubiri, mpenzi… (uk. 25)

Nukuu hii inaonesha hali ya utanzia baada ya wapenzi wawili waliopendana toka utotoni wakifa wakikumbatiana kwa sababu ya mapenzi. Kitendo kama hiki kipo katika jamii inayotuzunguka na watunzi wanatunga kazi zao katika kushabihikweli uliopo katika jamii husika.

Aidha, Mhusika Joram anakutana na hali ya kusikitisha baada ya kukutana na kipigo kikali kutoka kwa watu wasiojulikana. Na kujikuta akipatwa na maumivu makali kutokana na mateso hayo. Mtunzi anasema:

> Fahamu zilipomrudia polepole kinyume na zilivyomtoka. Zikafuatiwa na maumivu makali kichwani. Kisha, akasikia kitu kingine ambacho awali hakukisikia, mlio wa kitu kama pigo lililokuwa likirudiwa kumpiga kichwani kila baada ya muda Fulani. Pigo kubwa, zito, lenye maumivu ya aina yake, yenye baridi kali. Ukali wa baridi hiyo na kitisho cha mlio wa kipigo (uk 37).

Hapa mwandishi anatuonesha kuwa hali ya mateso aliyoyapata Joram haikuwa ya mara moja bali kila baada ya muda kipigo kilijirudia. Na kusababisha kupata maumivu makali katika mwili wake. Kitendo hiki cha kipigo husababisha hali ya utanzia kwa sababu mwili hukumbwa na maumivu makali. Pia, mwandishi anaonesha jinsi gani kitendo cha usaliti kinavyoweza kusababisha hali ya majozi kwa

jamii. Kitendo cha Askari jeshi kumsaliti Raisi wao na kusababisha kifo cha Raisi huyo. Mtunzi anasema:

> Sijaisahau hotuba hiyo, Joram. Sijaisahau kwani ilinishangaza sana kuona hotuba nzuri kama hiyo ikisababisha mauti ya mpendwa Pusi Ngokote. La kusikitisha zaidi ni kwamba aliuwawa na mmoja wetu. Mmoja kati ya watu walewale ambao alikuwa akiwatetea… (uk. 98).

Hapa inasawiri maisha ya jamii katika baadhi ya nchi ambazo kutokana tu na uchu wa madaraka wanatamani kuipindua serikali yao. Rais Pusi Ngokole aliuawa na baadhi ya askari wake ili kupata madaraka na kusababishaa utanzia katika jamii. Jambo hili linatokea katika jamii zetu ambalo linasababishwa na uchu wa madaraka au mali na kusababisha nchi kuingia katika machafuko ya kisiasa. Hivyo, mtunzi ametunga kazi yake katika kusawiri ukweli ulipo katika jamii. Aidha, hali hii ilimsababishiaa mmoja wa askari mzalendo kuingia katika kadhia. Askari wale baada ya kuona mwenzao hataki kuungana nao katika harakati zao, wakaamua kummaliza kwa kupiga risasi. Anasema:

> “Nini?” Nilinguruma. Nilipomtazama Ngokole nilizidi kuchanganyikiwa nilipomuona akitabasamu bila hofu yoyote. ‘Kwa nini? haiwezekani’ nikafoka tena, huku nikianza kufungua pingu zilizomfunga Ngokole mikononi. “Kitendo changu kiliwashangaza wakuu wangu. Walipopata fahamu nilishtukia nikipigwa singe matakoni. Nilipoinuka nimfuate mkuu huyo nilipata risasi ya ghafla ambayo ilipita jichoni. Nikaanguka na kuzirai (uk. 100).

Hapa mwandishi anaonesha jinsi gani dunia inavyokuwa na wabaya, lakini si wote wanaokubali kuifanyia nchi yao unyama. Kitendo alichokifanya askari mzalendo kilisababisha hali ya kusikitisha kwa kupoteza jicho moja. Wanajeshi wazalendo wapo katika jamii zetu ambao sio rahisi kuwadanganya kwa sababu ya mali au madaraka.

Katika riwaya hii, mwandishi anaendelea kuonesha mauaji ya kutisha ya watu wa nchi ya Ngokole. Tukio ambalo lilisababisha hali ya huzuni na kusikitisha. Baada ya

majeshi ya serikali kuwavamia watu waliokuwa wamekimbilia msituni kwa nia njema. Anasema:

> Niliona huo ni uharibifu mkubwa wa maisha. Nilipowatazama watu wawili watatu waliokuwa wakiugua kukata roho, nilijikuta nikitokwa na machozi ambayo niliyafuta mara moja na kujiunga na kazi ya kukusanya silaha na mavazi toka kwa wafu hao. Kazi ya mwisho ikawa kuwazika marehemu wote katika mashimo na mapango. Wafu wachache wa upande wetu tuliwazika kwa heshima zote zilizowezekana (uk. 107).

Nukuu hii inatuonesha namna matukio ya kivita yanavyoweza kuibua utanzia. Baada ya vita hivi watu walionekana wakiwa katika majeraha makubwa na wengine kupoteza maisha katika harakati za kujitetea. Aidha, matukio ya mauaji katika nchi ya Ngokole kwa watu wasio na hatia yaliendelea siku hadi siku. Ndugu wa watu ambao walikimbilia msituni walichukuliwa na askari wa serikali na kuteswa mpaka kufa kwao. Mtunzi anasema:

> Uovu mwingi ulifanywa kutulegeza mioyo. Kwa mfano, unionavyo hivi sina ndugu wala wazazi. Wote waliuwawa na majeshi ya serikali baada ya wapelelezi wao kunitumia barua ya vitisho na kunibembeleza wakinitaka nirudi mjini. Nilipokataa ndugu zangu walianza kuuawa mmojammoja kwa madai kuwa wanashirikiana na nami kutuibia siri. Nasikia baba na mama walikufa kwa taabu sana. Walichomwa visu mwili mzima, wakapakwa chumvi na pilipili na kisha kuanikwa juani ambako walikata roho baada ya kutaabika kwa muda mrefu (uk. 108).

Hapa inathibitisha wazi kuwa utanzia ambao upo katika riwaya hii ni wa umwagaji wa damu uliotokea katika nchi ya Ngokole. Katika jamii ya leo mauaji yanayotokana na uchu wa madaraka yameshamili na wanafasihi wameliona hili na kuandika matukio hayo katika kazi zao ili kuendana na mazingira halisi yanayoizunguka jamii. Kwa hiyo, hizo ni baadhi ya nukuu ambazo zimetumika katika riwaya ya *Dimbwi la Damu k*atika kuibua utanzia.

### 4.3.3 Riwaya Teule za Hussein Tuwa

Riwaya za Hussein Tuwa zilizotafitiwa ni *Mkimbizi* na *Mdunguaj*i. Maelezo yafuatayo ni kuhusu mawazo ya jumla ya kazi hizo.

#### 4. 3. 3. 1 Muhtasari wa Riwaya ya Mkimbizi

Riwaya ya *Mkimbizi* imechapishwa mwaka 2015. Riwaya hii ni moja kati ya riwaya zilizotumika katika utafiti huu kama data ya msingi. *Mkimbizi* ni riwaya inayosimulia kisa cha mwanadada Tigga Mumba. Tigga anashuhudia mauaji ya kutisha akiwa msituni alipokwenda na wenzake kufanya utafiti wa masalia ya kiumbe cha kale wilayani Manyoni. Bila ya kufikiri, anarekodi video ya mauaji yale kwa kamera. Mambo yanambadilikia ghafla pale anapojikuta akituhumiwa kuhusika na mauaji yale na kudaiwa kuwa alikuwa na matatizo ya ugonjwa wa akili uliomsukuma kufanya mauaji. Akiwa na uhakika kabisa kuwa hakuwa na ugonjwa wa akili na si aliyefanya mauaji yale, anaishiwa namna pale ambapo kila mtu, hata jamaa zake wa karibu kabisa, wanapoelekea kuamini kuwa ni yeye ndiye aliyefanya mauaji yale. Kinachofuata ni mkimbizano, hekaheka na taharuki. Wakati Tigga anatumia kila aliwezalo kuwakimbia wauaji wale wenye azma ya kumnyang'anya ushahidi ule na kumuangamiza. Pia, analazimika kuwakwepa wana usalama wanaomuwinda kuhusiana na tuhuma ya mauaji yale. Ndipo anajikuta anakuwa MKIMBIZI ndani ya nchi yake. Riwaya ya *Mkimbizi* ina sura 19 zilizoandikwa kwa kirumi. Aidha, mtunzi katika riwaya hii ametumia sana mbinu ya taharuki. Mandhari yaliyotumika katika riwaya hii ni ya mkoa wa Singida na jiji la Dar es Salaam.

#### 4. 3. 3. 2 Muhtasari wa Riwaya ya Mdunguaji

*Mdunguaji* ni riwaya inayohusu wapiganaji kumi, wakiwemo Watanzania watatu, wanaounda kikosi maalum cha Umoja wa Mataifa kilichotumwa kulinda amani

nchini Sierra Leone. Wanashambuliwa na mdunguaji aliyejificha katika msitu waliokuwemo. Sita kati yao wanauawa, mmoja baada ya mwingine, kwa kudunguliwa na mdunguaji huyo hatari. Ni Mtanzania mmoja tu ndiye anayerudi nchini akiwa hai. Miaka mitatu baadaye mpiganaji aliyeshinda vita vingi vya msituni, Baddi Gobbos anajikuta akikabiliana na vita vingine katikati ya jiji la Dar es Salaam, pale anapojikuta akiwindwa na wauaji asiowajua. Wakati huo huo, Baddi anajikuta akiwa mateka aliyeshindwa katika vita vigumu kuliko vyote alivyowahi kukabiliana navyo maishani mwake… "Vita vya mapenzi." *Mdunguaji* ni riwaya ambayo imetumia muundo changamano katika kusimulia matukio yake huku ikijadili mambo muhimu kama vile matatizo ya kisiasa, usaliti, tamaa na mapenzi.

Riwaya hii ina mparaganyiko mkubwa wa mpangilio, matukio yake yamesukwa kwa mchanganyiko wa vita vya Sierra Leone, machafuko ya kisiasa nchini Liberia na athari zake, usaliti na uzalendo. Na vyote vinabadilishana nafasi kwa kwenda mbele na kurudi nyuma. Riwaya ya *Mdunguaji* imegawanyika katika sura 13 zilizoandikwa kwa tarakimu. Katika riwaya hii kumeonyeshwa jinsi matukio ya machafuko ya kisiasa yanavyoathiri taifa kwa ujumla. Mwandishi anatilia mkazo hali halisi ya mwanadamu ndani ya mfumo wa kisiasa na masahibu yanayompata mtu au kikundi cha watu au hata jamii na taifa kwa jumla linapokuwa limeshikwa ndani ya utando wa mfumo huo na huku kila mmoja akijipigania mwenyewe.

### 4. 3. 4 Matukio ya Kitanzia katika Riwaya za Hussein Tuwa

Sehemu hii inabainisha matukio yenye kuibua utanzia katika riwaya mbili za mwandishi Ben Mtobwa ambazo ni *Mkimbizi* na *Mdunguaji.*

#### 4. 3. 4. 1 Matukio ya Kitanzia katika Riwaya ya Mkimbizi

Matukio ya kitanzia katika riwaya ya *Mkimbizi* yamejitokeza kwa kiasi kikubwa kutokana na maudhui ya riwaya husika kama ifuatavyo:

Mwandishi anabainisha tukio la kitanzia la mauaji ambalo limetokea katika msitu huko wilayani Manyoni. Muuaji alikuwa akitumia bunduki kumaliza raia wasio na hatia. Mtunzi anasema:

> "Mamaaa!" Nilijisemea mwenyewe kwa woga huku nikiinua kamera kuangalia kule alipokuwa akikimbilia yule mwenyeji na hapohapo nilishuhudia yule mtu akitupa mikono yake hewani na kupiga yowe kubwa huku akipiga hatua tatu zaidi za kupepesuka na doa kubwa jekundu likitokea kwenye mgongo wa fulana yake iliyopauka. Alianguka chini kama mzigo na kufurukuta kidogo kisha akatulia. Amekufa!... Risasi kutoka kwenye bastola ya macho ya nyoka ilimpata katikati ya uti wa mgongo na kumuua papo hapo (uk. 14)

Nukuu hii inaonesha hali ya kuhuzunisha kutokana na kifo cha mwenyeji ambaye alikuwa anakimbia kuyanusuru maisha yake. Tukio kama hili la watu kuamua kuwaua wenzio kutokana na kuonekana katika shughuli zao za uarifu sio geni katika jamii yetu. Watunzi kutokana na kuliona hilo wanatunga kazi zao ili kusawiri maisha halisi ya jamii. Aidha, mwandishi anaendelea kueleza tukio jingine la kitanzia kwa kumtumia mhusika Ibrahimu Geresha ambaye alikutwa na umauti baada ya kupigwa risasi katikati ya paji lake la uso na kusababisha kifo chake. Anasema:

> Ibrahimu Geresha alikuwa amelala chali mbele ya hema lake huku akiwa ametumbua macho na amekenua meno kwa uchungu. Damu ilikuwa ikichuruzika kutoka katika tundu moja lilokuwa katikati ya paji lake la uso. Nilimkimbilia na kujibwaga ubavuni… Hatua chache kutoka pale alipoangukia bosi wangu Ibrahim Geresha niliona mwili wa yule mwenyeji mwingine tuliyepewa na ofisi ya mkuu wa wilaya nao ukiwa umeanguka pale kwenye ile ardhi ya mawe ukiwa hauna uhai tena (uk. 23).

Nukuu hii inaonesha jinsi gani mhusika alipata maumivu makali kabla ya kifo chake. Hali ambayo inaleta huzuni na masikitiko. Hii inayoonesha ni kwa namna gani mwandishi aliitumia kalamu yake vizuri katika kuibua matukio ya kitanzia

yanayosawiri maisha halisi ya jamii yetu. Pia, tukio kama hili la kuhuzusha limeibuliwa kwa kumtumia mhusika Beka. Kifo cha Beka ni cha kusikitisha, alipigwa risasi chini ya jicho lake la kulia na kusababisha damu nyingi kumwagika. Mtunzi anasema:

> Nilipotokeza mbele ya lile gari tu nilipata mshtuto mkubwa na yowe la woga likanitoka. Hapo hapo nilianza kupiga kelele kwa kiwewe huku nikikimbia hatua kadhaa kutoka kwenye lile gari. Beka alikuwa amelalia boneti la gari kwa ubavu wake huku mkono wake mmoja ukiwa umenyooshwa mbele, juu ya lile boneti na kichwa chake akiwa amekilaza juu ya mkono ule… Damu nyingi ilikuwa ikimtiririka Beka kutoka kwenye jeraha la risasi lilokuwa chini kidogo ya jicho lake la kulia (uk. 25).

Hapa mwandishi anaonesha namna matukio haya ya mauaji yanavyosikitisha. Beka alipigwa risasi na wauaji ili asije akatoa siri ya mtu waliyekuwa naye pale msituni. Tukio hili la kusikitisha linatokea pia, katika jamii zetu baada ya watu wabaya kugundua kuwa kuna mtu anajua siri zao chafu. Aidha, mwandishi anaendelea kuibua matukio ya kitanzia yaliyosababishwa na mauaji kwa kumtumia mhusika Gil. Anasema:

> Lilikuwa jambo ambalo sikulitegemea na la kutisha sana… Uso wa Gil ulikuwa ukinitumbulia macho bila kuona, kama vile alikuwa amelala kichwa chini miguu juu, nilikiri moyoni mwangu kuwa kwa hakika sasa nilikuwa nimeshindwa. Gil alikuwa ameuawa akiwa ndani ya gari, bila shaka akijaribu kutoroka kutoka eneo lile. Mwili wake ulikuwa umelala chali kwenye sakafu ya gari, kisogo chake kikiwa kimeegemea mlango wa dereva kwa ndani ambapo nilipofungua kichwa kile kiliangukia nje na kubaki kikining’inia wakati kiwiliwili chake kikibaki ndani ya gari (uk. 26).

Nukuu hii inaonesha hali ya huzuni na kusikitisha inayotokana na kifo cha Gil. Gil alikutwa ameuawa ndani ya gari. Kifo chake kilikuwa cha kuhuzunisha mno kutokana na kichwa chake kilikuwa kikining’nia nje wakati kiwiliwili chake kikibaki ndani ya gari. Vilevile, mwandishi ameibua tukio la kitanzia lililosababishwa na kitu chenye kuleta maumivu katika mwili wa binadamu. Kitu ambacho huweza

kusababisha hali ya masikitiko na kuhuzunisha. Akimtumia mhusika Tigga ambaye anachomwa na kitu kama sindano katika ubavu wake wa kulia, mtunzi anasema:

> Ghafla nilisikia nikichomwa na kitu kama sindano kwenye ubavu wangu wa kulia na hapo hapo nilihisi maumivu makali na mwili wangu ukinifa gazi kutokea kiunoni kuelekea chini. Nilijishika eneo lililochomwa huku nikitoa yowe la uchungu na kuangaza huko na huko nikimtafuta aliyenichoma… Nilihisi kichwa kikiniwia chepesi na miguu ilianza kugongana, ilhali kizunguzungu kikinigubika ghafla (uk. 175).

Tukio hili linaonesha maumivu ambayo mtu anaweza kuyapata baada ya kuchomwa na kitu chenye madhara kwa binadamu. Tigga anapata maumivu makali katika mwili wake baada ya kuchomwa na kitu kisichojulikana. Tukio kama hili lipo katika jamii kutokana na watu kutumia vitu mbalimbali kuwadhuru wengine kutokana na sababu zao. Hivyo, watunzi wanatunga kazi zao kutokana na matukio halisi yanayoendelea katika jamii. Mwandishi anabainisha tukio lingine ambalo linaibua hali ya utanzia katika jamii. Tukio la kulazimisha kufanya jambo fulani bila kutaka na kama ikitokea umekataa, madhara makubwa yanakufika. Mtunzi anasema:

> Hatimaye nilimweleza raisi ukweli wa jambo lote, na kujiuzuru nafasi yangu ya utabibu wa rais. Rais alianzisha msako mkali wa kuwasaka mke na watoto wangu waliotekwa na wale watu ambao niliwajua kwa sura lakini sikuyajua majina yao. Kitendo hicho kiliwaudhi sana wale watu na siku moja baada ya kujiuzuru nafasi yangu, mwili wa mke na watoto wangu ilionekana kando ya msitu mmoja tayari wameuawa (uk. 212).

Nukuu hii inaonesha jinsi gani jamii yetu ilivyojaa vitisho na ukatili mkubwa. Tukio la kuuwawa kwa mke na watoto wa Daktari Kashushu baada ya kukataa kumuwekea dawa ambayo baadaye angekuwa chizi ni la kuhuzunisha na kusikitisha. Aidha, mwandishi anaendelea kuibua matukio ya kitanzia ambayo yanayosababishwa na ugonjwa hatari wa saratani. Anasema:

> "Engagement? Ina maana sikuwa na mchumba?" Nilimuuliza. Kemirembe aliguna na kutabasamu kwa kukata tamaa. *"She died of cancer two month later".* Mungu wangu! Nilijishika mdomo kwa masikitiko juu ya habari ile. "Eeenh, ndio Mungu huyo! Baada ya hapo Kristus alikufa moyo kabisa. Alichukua likizo bila malipo ofisini kwake, na kubaki akilala tu nyumbani kwake (uk. 253).

Hapa, mwandishi anaonesha jinsi magonjwa kama vile saratani yanavyosababisha hali ya kusikitisha na kuhuzusha kwa jamii. Mbali na kuumwa kwa muda mrefu pia, huweza kusababisha kifo. Ugonjwa huu upo katika jamii ambao unasababisha huzuni na simanzi kwa jamii. Hivyo, mtunzi ametunga kazi yake kwa kusawiri magonjwa halisi yaliyomo katika jamii. Aidha, mwandishi anaendelea kuibua matukio ya kitanzia kwa kumtumia Khelef Janabi. Khelef anauwawa nyumbani kwake na mtu asiyejulikana. Anasema:

> Hatua chache mbele yangu pale sakafuni, niliona dimbwi la damu na mchirizi mnene wa damu, kana kwamba mtu aliyetoka damu ile alisota au alivutwa kuelekea kwenye korido… Niliufuata ule mchirizi mnene wa damu ambao uliniongoza hadi kwenye chumba cha kulala. Nilimkuta akiwa amelalia ubavu sakafuni, kiasi cha hatua moja tu kutoka kwenye kitanda cha kulalia. Shuka jeupe lililotandikwa kitandani pale likiwa na doa baya la alama za vidole vyenye damu. Pale sakafuni, damu kidogo ilikuwa imetambaa kutokea usawa wa kifua cha yule mtu ambaye niliamini kuwa ni Khelef Janabi (uk. 280).

Hapa mwandishi anaonesha hali ya huzuni ambayo imesababishwa na kifo cha Khelef Janabi ya kujehuriwa kifuani kwake.Vilevile, tukio la kutegewa bomu linaweza kuibua hali ya utanzia kwa jamii. Mwandishi amemtumia mhusika Jaji Reuben katika kuibua tukio la kitanzia baada ya gari lake kulipuliwa na bomu lililotegwa bila yeye kujua. Mtunzi anasema:

> Nilikuwa nikiendelea kulitazama lile gari likiondoka eneo lile kwa ghafla niliposikia mlipuko mkubwa sana uliotikisa ardhi na majengo ya maeneo yote ya eneo lile, na wakati huo huo nilishuhudia kwa kihoro kikubwa lile gari likitawanyika vipande vipande na moto mkubwa ukiruka kutoka sehemu ya mbele ya gari lile sambasamba na mlipuko ule… Gari la Jaji Reuben lilikuwa likiendelea kuteketea kwenye moto mkubwa. Hakukuwa na uwezekano wa yeye wala yule dereva wake kupona kwenye mlipuko ule (uk. 295).

Nukuu hii inaonesha hali halisi katika jamii kwa sababu jamii inashuhudia matukio mengi ya kitanzia yanayosababishwa na mabomu ndani na nje ya nchi. Hivyo, watunzi wanatumia matukio halisi na kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Kwa hiyo, haya ni baadhi ya matukio yaliyotumika katika riwaya ya *Mkimbizi* katika kuibua utanzia.

#### 4. 3. 4. 2 Matukio ya Kitanzia katika Riwaya ya Mdunguaji

Katika riwaya ya *Mdunguaji* kuna matukio mbalimbali yanayoibua utanzia. Matukio ambayo yametokana na vita vya kisiasa na tamaa ya mali. Hivyo basi, matukio mengi yanayoibua utanzia ni ya mauaji. Mwandishi anasema:

> Wakati huohuo alihisi akipigwa na kitu kizito na akitupwa hadi katika dimbwi la maji. Alijipindua haraka akiwa tayari kujibu mashambulizi, lakini adui hakuonekana… Jina la uficho Cheetah alikuwa amelala chali kando ya dimbwi dogo la maji akiwa ametawanya miguu na mikono yake kila upande. Kichwa chake kilikuwa kimezama ndani ya lile dimbwi dogo la maji ilhali mwili wake ukiwa umetulia tuli. Hakukuwa na shaka kabisa miongoni mwa wapiganaji wale kuwa mwenzao mmoja alikuwa ameuawa kwa risasi (uk. 5).

Hapa, mwandishi amemtumia mhusika Cheetah wa Sierra Leone ambaye amepigwa risasi na mdunguaji katika harakati za kupambana naye. Cheetah anapoteza maisha katika harakati hizo na kusababisha hali ya huzuni. Tukio kama hili la mwanajeshi kuuwawa wakati wa mapambano ya kivita na kusababisha utanzia lipo katika jamii. Hivyo, mtunzi ameandika kazi yake ambayo inasawiri maisha halisi ya jamii. Aidha, mwandishi anaendelea kuibua utanzia katika uwanja wa vita ambapo mdunguaji anaendelea kuwamaliza adui zake mmoja baada ya mwingine. Anasema:

> Risasi ilipita milimita chache juu ya bega la Black Angel na kujikita kifuani kwa Angle. Yowe kubwa lilimtoka yule mpiganaji huku akiachia machela aliyekuwa amebeba na mwenzake, naye akitupwa nyuma kwa msukumo wa risasi ya mdunguaji. Kizaazaa kiliamka upya msituni, Mdunguaji bado alikuwa anaendelea na mashambulizi yake ya kuvizia… Black Angle alimtupia macho Angle aliyekuwa anagaagaa chini huku akilia kwa uchungu akiwa amejishika kifuani

> ambapo risasi imempata. Damu ikimchuruzika kutoka kwenye vidole vyake na mdomoni, macho yakiwa yamemtoka kwa woga mkubwa kabisa. Alijaribu kujiinua lakini alishindwa (uk. 12).

Tukio lingine la kuhuzunisha linalotokana na mapambano ya kivita katika msitu linamuhusu mhusika huyohuyo, Black Angle. Mwandishi anasema:

> Muda huohuo Black Angle alitupwa hewani, bunduki yake ikimtoka na kubwagwa chini akiwa maiti. Risasi ya mdunguaji ilimpata sawia katikati ya paji  la uso, naye alipatwa na mshtuko hakuweza hata kupiga yowe… Mwili wa Black Angle ulilala ukiwa hauna uhai hatua kadhaa kutoka pale ulipolala mwili wa Angle. Wapiganaji wanne wa kikosi maalum cha Umoja wa Mataifa walikuwa wameuawa (uk. 14).

Nukuu hizi mbili zinaonesha jinsi matukio haya yanavyoibua utanzia. Kitendo cha kuuwawa kwa wapiganaji hao wa kulinda amani nchini Sierra Leone ni cha kusikitisha na kuhuzunisha.Vile vile, mwandishi anaendelea kuibua utanzia akimtumia mhusika Vampire. Vampire alipigwa risasi na mdunguaji na kujikuta akipatwa na maumivu makali. Tukio hili husababisha hali ya kusikitisha. Anasema:

> Alifyatua risasi huku akijitupa pembeni. Wakati huohuo alihisi maumivu makali upande wa kulia wa kifua chake, huku akihisi kitu kama msumari wa moto ukiuingia mwili wake na kutembeza ganzi upande wake wote wa kulia. Alitupwa hewani, ile ganzi ikitoweka haraka na maumivu makali yakiutawala mwili wake. Alipigiza mgongo wake kwenye jiwe kubwa lililokuwa karibu yake na kuserereka kuangukia kule kwenye mporomoko mkali… (uk. 40).

Hapa mwandishi anaonesha Vampire alivyokuwa katika wakati mgumu baada ya kupigwa risasi na mdunguaji, na kuangukia mgongo katika jiwe kubwa. Kitendo ambacho kilisababisha kupata maumivu makali katika mwili wake, hali ambayo inasikitisha. Pia, tukio lingine la mauaji lililoibua hali ya utanzia ambayo mwandishi amelitumia ni mauaji ya Alpha na Black Mamba. Alpha amekufa kifo cha kusikitisha baada ya kichwa chake kufumuliwa kwa risasi kutoka kwa Vampire, na Black Mamba kuuwawa na Mdunguaji. Mtunzi anasema:

> Black Mamba alipiga kelele huku akishuhudia kwa kiroho wakati kichwa cha mpiganaji kutoka Tanzania aliyemtambua kwa jina la uficho Alpha kikitawanywa vibaya sana na risasi kutoka kwenye

> bastola ya Vampire na kuanguka chini kama gunia… Alijitupa chini na kugeukia kule alipoangukia Vampire na kumuona akiwa ametapakaa damu kifuani huku akijitahidi kujishikilia kwenye jiwe kubwa kwa mkono wake wa kushoto… Pale alipoling'ang'ania lile jiwe, Vampire alikuwa katika maumivu makali damu nyingi ilikuwa ikimtoka na alihisi fahamu zikimpotea… (uk. 42).

Nukuu hii inaonesha kwa namna gani tukio hili linavyoleta huzuni kwa msomaji. Kitendo cha kutawanywa kwa kichwa cha Alpha na maumivu aliyopata Vampire baada ya kuangukia jiwe ni cha kusikitisha na kuhuzunisha. Pia mwandishi anaendelea kubainisha matukio ya kitanzia katika riwaya ya *Mdunguaji*. Anasema:

> Aliinua uso wake kwa woga na kutaka kumpigia kelele Black Mamba lakini alipigwa na butwaa na kihoro kikubwa zaidi pale alipoona kichwa cha Black Mamba kikitawanyika vibaya sana na kiwiliwili chake kikianguka chini kama mzigo… Kutokana na ukaribu aliokuwako mdunguaji, ile risasi iliking'oa kabisa kichwa cha Black Mamba kutoka kwenye kiwiliwili chake na kukitawanya vipande vipande, damu, mapande ya nyama na ubongo vikitupwa kila upande (uk. 43)

Nukuu hizi mbili zinabainisha matukio ya kitanzia yanavyoweza kuibuliwa na mwandishi kwa msomaji. Kifo cha Alpha ni cha kusikitisha ingawa alikuwa msaliti, Black Mamba pia kifo chake kilihuzunisha zaidi kwani alikuwa mpiganaji mzalendo. Matukio ya namna hii ya kutisha na kutia simanzi yapo katika jamii zetu, ambayo wanakutana nayo wanajeshi kipindi cha vita na kusababisha utanzia mkubwa kwa jamii husika.

Pia, mwandishi anaibua tukio lingine la kuhuzunisha baada ya kumtumia mhusika Gilda. Gilda anapatwa na tukio la kusikitisha baada ya wauaji kutaka kumchoma kisu Vampire na Gilda kutaka kumsaidia, na hatimaye kisu kumpata yeye na kupelekea hali yake kuwa mbaya na kulazwa hospitali ya M-uhimbili. Anasema:

> "Baddi!" Gilda aliita kwa uchungu, na ndipo kwa mara ya kwanza Baddi alipohisi unyevu mikononi mwake. Alimtazama Yule binti na akahisi ubaridi ukimtambaa mwili mzima pale alipoona sehemu ya mbele ya nguo ya Gilda ikiwa imetapakaa damu hali mpini wa kisu ukiwa umechomoza kifuani kwa yule dada, upande wa kushoto. Kile

> kisu kilikuwa kimemdhamiria yeye, na Gilda, katika kujaribu kumsukuma pembeni, akajiweka katika njia ya kisu kile na matokeo yake kimejikita kifuani kwake (uk 125).

Hapa mwandishi anaonesha tukio la kusikitisha la kuchomwa na kisu. Gilda katika harakati za kumkinga Vampire anajikuta akidhurika yeye, hali ambayo imesababisha masikitiko. Tukio hili la kutetea uhai wa mtu mwingine na kuweka wa kwako hatarini lipo katika jamii. Hii inatokana na kuona umuhimu wa mtu huyo kuliko wako na kujikuta unafanya kitendo kama hiki cha kijasili. Hivyo, katika dondoo hizi zote watunzi wameonesha matukio mbalimbali ambayo huweza kuibua utanzia kwa jamii.

## 4. 4 Kufanana na Kutofautiana kwa Utanzia Uliomo katika Riwaya za Waandishi Teule

Mara kwa mara utanzia ni sehemu ya maisha ya kila siku. Ni kawaida hisia kukabiliana na hasara za kimwili na kisaikolojia. Kila mtu ameathirika tofauti tofauti kutokana na sababu za ndani au za nje ambazo zinaweza kupelekea utanzia. Utanzia si ugonjwa wa akili, bali ni hisia ambayo inaweza kuwa kwa dakika chache, siku chache au kwa miaka michache. Sehemu hii inalinganisha na kulinganua utanzia uliomo katika riwaya za waandishi teule. Hoja kuu hapa ni kuthibitisha kwamba utanzia uliomo katika riwaya za Ben Mtobwa na Hussein Tuwa unalandana na kutofautiana kwa namna moja ama nyingine. TUKI (2004) wanasema kuwa ulinganishaji ni hali ya kuwa sawa, uwiano, ulingano au urari wa jambo au kitu fulani na kulinganua ni kueleza au kutaja sifa za vitu viwili ili kuonesha tofauti zake. Kwa hiyo, hapa tutajadili kulinganisha na kulinganua kazi za waandishi teule.

### 4. 4. 1 Kufanana kwa Utanzia Uliomo katika Riwaya za Waandishi Teule.

Hapa tunalinganisha kwa kujigeza maeneo mawili ambayo ni aina za utanzia na malengo ya utanzia katika kazi za waandishi teule.

#### 4. 4. 1. 1 Kufanana kwa Aina za Utanzia

Watunzi wote wawili wametumia aina mbili za utanzia kati ya tatu zilizojadiliwa katika tasnifu hii, yaani utanzia wa kisaikolojia na kimwili. Mwandishi Ben Mtobwa ametumia utanzia wa kisaikolojia katika riwaya ya *Dimbwi la Damu* katika kuibua hali ya utanzia kwa msomaji. Anasema:

> Nimeamua kujiua baada ya kuuona uovu nilioutenda kwa jamii yangu. Uovu wangu ndio kisa cha kifo cha Maimuna na Juma. Kwa kweli, sidhani kama nafanya makosa kujua. Sistahili kuishi hata kidogo. Nimejaribu kujiua kwa kujikata koo kwa kisu, nimeshindwa. Hata hivyo, sikubali kujisamehe. Nimeamua kwenda ziwani ambako nitaogelea, niogelee hadi nichoke, nishindwe kurudi. Kama samaki hawatanila maiti yangu, mtaokota mzoga wangu ukielea majini. Nizikeni pamoja na waovu wengine (uk.40).

Nukuu hii inaonesha mtunzi alivyotumia utanzia wa saikolojia. Mhusika Bob alikumbwa na huzuni kutokana na maovu aliyoyatenda mpaka kusababisha vifo vya wapendanao Maimuna na Juma. Kutokana na kujikuta hana raha, mawazo yanamsumbua anaamua kujiua mwenyewe kwa kujitosa ziwani. Kitendo ambacho kipo katika jamii halisi.

Aidha, Ben Mtobwa anaendelea kudhihirisha hili katika riwaya ya *Najisikia Kuua Tena* akimtumia mhusika Inspekta Kombora ambaye anahuzunika kutokanana mauaji yanayoendelea katika nchi yake. Anasema:

> “Isinitishe!” Kombora alifoka. Kisha alijirudi na kujaribu kutabasamu, lakini tabasamu halikutokea. Akamtazama Abdala kwa huzuni huku akiwaza; Huyu hajui. Hafahamu kuwa napata simu za mauuji kila kabla ya mauaji hayo. Naweza kustarehe vipi, mimi kama kiongozi

> wa polisi, hali muuaji ananikebehi kwa siku kabla ya kumwaga damu isiyo na hatia? (uk. 39).

Hapa mwandishi ametumia utanzia wa kisaikolojia kutokana na tatizo linalomnyima raha Inspekta Kombora. Kombora anakuwa katika wakati mgumu kutokana na vifo vya watu wasio na hatia vinavyoongezeka. Mbaya zaidi muuaji anampigia simu na kumwambia maneno ya dhihaki. Jambo hili lipo katika jamii na inatokana na kuwa na mapenzi ya kazi.

Vilevile, Hussein Tuwa ametumia aina hii ya utanzia katika riwaya zake teule. Katika riwaya ya *Mkimbizi* mwandishi amemtumia mhusika The Bastard baada ya kupokea kifo cha Kristus. Anasema:

> "Nasikitika sana dada yangu, lakini nimeshuhudia kwa macho yangu Mr. Kristus akiuawa" Nilimjibu kwa upole. The Bastard alionekana kuchomwa waziwazi na yale maneno na akafinya macho na kushika kifua chake sehemu ambayo moyo ulikuwepo na kujikunja kwa uchungu. Kilio cha uchungu cha kimya kimya kilimtawala, nami niliona tu mwili wake ukitikisika kwa kila wimbi la kilio lililomtoka... Ilikuwa ni taswira ya kuhuzunisha sana na kujikuta nikijilazimisha kutazama pembeni huku nami nikitiririkwa na machozi (uk. 252).

Nukuu hii inaonesha kwa namna gani Bastard alihuzunika kisaikolojia baada ya kupokea taarifa cha kifo cha mdogo wake Kristus. Aidha, mwandishi ameonesha aina hii ya utanzia katika riwaya ya *Mdunguaji* akimtumia mhusika Baddi. Anasema:

> Kwa mara nyingine tena, Baddi alitikisa kichwa kwa kukata tamaa. Alihisi kusalitiwa kwa kiasi kikubwa kabisa. Yaani siku zote alivyokuwa akikabiliana na mashaka mazito huko ughaibuni ilikuwa ni kwa ajili aendelee kuishi ili hatimaye aje akutane tena na familia yake, sasa tena anaporejea hapa nchini anagundua kuwa kumbe vyote alivyokuwa akivipigania akiwa huko ughaibuni havipo tena kwa ajili yake. Taratibu Baddi aliinuka na kusimama. Alivuta punzi ndefu na kuzishusha huku akijifuta machozi (uk. 192).

Hapa mtunzi amemtumia mhusika Baddi baada ya kutoka vitani kurudi nyumbani mambo yamebadilika. Kwanza baba yake mzazi amefariki dunia na mkewe ameolewa na mume mwingine tena mume mwenyewe ni bosi wake aliyemtuma kazi

ya kwenda vitani. Kitendo hiki kinamuharibu kisaikolojia na kuamua kuondoka bila kuaga. Pia, waandishi wote wawili wametumia utanzia wa kimwili katika riwaya zao teule. Kwa mfano, Ben Mtobwa katika riwaya ya *Dimbwi la Damu* amemtumia mhusika Joram. Anasema:

> Fahamu zilipomrudia polepole kinyume na zilivyomtoka. Zikafuatiwa na maumivu makali kichwani. Kisha, akasikia kitu kingine ambacho awali hakukisikia, mlio wa kitu kama pigo lililokuwa likirudiwa kumpiga kichwani kila baada ya muda fulani. Pigo kubwa, zito, lenye maumivu ya aina yake, yenye baridi kali. Ukali wa baridi hiyo na kitisho cha mlio wa kipigo (uk 37).

Hapa mwandishi ameonesha utanzia wa kimwili ulivyojitokeza. Joramu anapatwa hali ya huzuni baada kupata kipigo kutoka kwa watu wasiojulikana na kumsababishiwa maumivu makali kwenye kichwa. Pia, Hussein Tuwa ametumia aina hii ya utanzia katika riwaya ya *Mkimbizi.* Anasema:

> Moja kwa moja Macho ya Nyoka alimwendea yule mtu, alimwiinua kikatili na kumkalisha kitako huku miguu yake iliyofungwa kamba ikiwa imenyooshwa mbele... Tendo lile lilimkera macho ya nyoka na kuanza kumvurumishia kipigo kikubwa yule mtu, mateke, ngumi makofi. Yule mtu asiye na jina alibaki akigaragara mchangani kwa uchungu na maumivu makubwa (uk 15).

Nukuu hii inaonesha kwa namna gani maumivu ya kupigwa yanavyoweza kusababisha hali ya huzuni kwa mhusika. Kwa hiyo, waandishi wote wawili wameweza kutumia aina hii ya utanzia katika kazi zao kwa kiasi kikubwa.

#### 4. 4. 1. 2 Kufanana kwa Malengo ya Utanzia

Waandishi wote wawili wanafanana katika malengo ya utanzia katika riwaya teule. Kwanza wote, kwa maoni yetu, walikuwa wanalengo la kuonesha matukio yanayoibua huzuni kwa jamii ambayo ni usaliti, vifo, ajali, mapenzi na mengine yanayofanana na hayo. Kwa mfano, katika riwaya ya *Najisikia Kuua Tena* mtunzi amemtumia mke wa Wamangi baada ya kutokea kifo cha mumewe. Anasema:

> Mume wangu mpenzi alikuwa kalala chali kitandani, uchi kama alivyolala usiku wa jana, mwili wake mzima ukiwa umeloa damu nzito ambayo ilikuwa ikiendelea kutiririrka kutoka katika jeraha baya mno la kisu au sime lilokuwa wazi kifuani. Sikuweza kutazama mara mbili. Nadhani nilianguka na kuzirai (uk. 35).

Hapa mwandishi alikuwa ana lengo la kuionesha jamii kwa kiasi gani tukio la kifo linavyoweza kuibua simanzi kwa jamii husika. Kitendo hiki kipo katika jamii zetu ambacho kinawakumba watu wengi baada ya kufiwa na watu wao wa karibu. Pia, Hussein Tuwa ameonesha jambo hili katika riwaya yake ya *Mkimbizi.* Anasema:

> Oh! Kelvin. Hivi ni kweli sasa umelala chini ya udongo huu? Chozi lilinivuja na nikahisi moyo ukiniuma sana. Nilijaribu kumsalia Kelvin lakini sikuwa na kumbukumbu ya sala yoyote ya kumuombea. Nilibaki nikimeza funda la mate kulainisha koo langu ambalo lilikuwa limeshika na donge kubwa (uk.300).

Nukuu hii inaonesha kuwa mwandishi ametumia tukio hili la kufa ili kuibua utanzia kwa jamii. Tigga alihuzunika baada ya Mchumba wake Kelvin kuaga dunia. Hivyo, waandishi wote wawili walikuwa na lengo la kuonesha ni matukio yapi yanayoibua utanzia.

Vilevile, waandishi wote wawili wana lengo la kuushambulia uovu wa viongozi walio madarakani au vigogo wenye uwezo kifedha. Ben Mtobwa amemtumia Bob na Kwame kuonesha uovu wa watu wenye fedha wanavyotumia vibaya kuwaumiza wengine. Pia, amewatumia maaskari wa nchi ya Ngoko waliokuwa tayari kumsaliti Raisi wao kutokana na uchu wa madaraka. Aidha, Hussein Tuwa amewatumia akina Wagga watu wenye uwezo kifedha wanavyowatendea unyama watu wasio na hatia. Pia, amemtumia askari mwanamke na Jaji Obeid kuonesha kwa namna gani watumishi wa serikali wanavyotumia madaraka yao kuwakandamiza wengine.

### 4. 4. 2 Kutofautisha Utanzia katika Riwaya za Waandishi Teule

Mjadala wa tofauti za utanzia wa waandishi teule umefanywa kwa kujigeza katika maeneo mawili ambayo ni idadi ya matukio ya kitanzia na mtazamo. Ufuatao ni ufafanuzi wa tofauti hizo:

#### 4. 4. 2. 1 Tofauti ya Idadi ya Matukio ya Kitanzia

Riwaya teule zinatofautiana katika idadi ya matukio yanayoibua utanzia. Riwaya za Ben Mtobwa zina kiasi kidogo cha matukio yanayoibua utanzia. Hii inatokana na ukweli kuwa riwaya zake ni fupi kuliko riwaya za Hussein Tuwa. Katika riwaya ya *Najisikia Kuua Tena* ina jumla ya kurasa 119 na sura 19 na katika riwaya ya *Dimbwi la Damu* ina jumla ya kurasa 115 na sura 7. Wakati riwaya za Hussein Tuwa ni ndefu kuliko za Ben Mtobwa. Riwaya ya *Mkimbizi* ina jumla ya kurasa 394 na sura 19 na katika riwaya ya *Mdunguaji* kuna jumla ya kurasa 325 na sura 13. Kwa hiyo, kuna tofauti ya wazi katika idadi ya matukio ya kitanzia katika riwaya teule kutokana na kutofautiana kwa ukubwa wa kazi husika.

#### 4. 4. 2. 2 Tofauti ya Kimtazamo

Ben Mtobwa katika riwaya zake anaonesha kwa jinsi gani wazalendo wanavyoitajika katika nchi, na kuonesha kwa wazi kabisa jinsi alivyokuwa anakerwa na watu wanaopenda mapinduzi. Kwa kumtumia mhusika Joram, anaonesha kuwa katika nchi wanahitajika wazalendo katika kupigania taifa. Wakati Hussein Tuwa yeye anangalia dunia katika hali iliyojaa tamaa kuliko uhai wa mtu. Yeye anaona binadamu wa sasa wanathamini sana pesa kuliko maslahi ya watu wengine.

### 4. 4. 4 Muhtasari wa Sura ya Nne

Sura hii ya nne imejihusisha na uwasilishaji na uchambuzi wa data kutokana na malengo ya utafiti. Aidha, imebainisha vijenzi vya utanzia, aina za utanzia, matukio ya kitanzia yaliyomo katika riwaya teule pamoja na kufanana na kutofautiana kwa utanzia uliomo katika riwaya za waandishi teule

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5. 1 Utangulizi

Sura hii inabainisha muhtasari, hitimisho pamoja na mapendekezo ya utafiti zijazo. Katika hitimisho tumefafanua utoshelevu wa mkabala uliotumika katika uchambuzi wa data pamoja na mchango mpya wa utafiti.

## 5. 2 Muhtasari

Utafiti uliofanyika ulilenga kuchunguza matumizi ya utanzia katika riwaya pendwa za Kiswahili: Ulinganisho wa Ben Mtobwa na Hussein Tuwa. Riwaya zilizotumika ni *Najisikia Kuua Tena, Dimbwi la Damu, Mkimbizi na Mdunguaji*. Tumechunguza na kubainisha matukio ya kitanzia yalivyojitokeza katika riwaya zilizoteuliwa na jinsi gani yanavyohusiana na jamii. Aidha, kulinganisha na kulinganua utanzia katika riwaya pendwa za waandishi teule. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Uhalisia. Mawazo ya mwanahalisia Wamitila ndiyo yaliyotumika kwa kiasi kikubwa katika utafiti huu kwa kuzingatia mambo halisi yanayotokea katika maisha ya binadamu.

Tasnifu hii imejengwa na sura tano: Katika Sura ya Kwanza, tumeweka msingi wa tasnifu hii kwa kutoa usuli wa tatizo la utafiti na tamko la utafiti. Tumeeleza pia malengo, maswali na umuhimu wa utafiti huu. Kiunzi cha nadharia pamoja na mapitio vimejenga sura ya pili. Sura ya tatu imejumuisha mbinu za utafiti za ukusanyaji data, uchakataji data, sampuli na mahali ulipofanyika utafiti. Mbinu ya kukusanya data maktabani na uwandani, uchakataji kupitia utafiti usio wa kiidadi utumiao maelezo vimeelezwa. Pia, uchaguzi wa sampuli kupitia sampuli lengwa ilitumika katika utafiti umefafanuliwa. Uwasilishaji na mjadala wa data katika

kujenga sura ya nne ya tasnifu hii. Ni katika sura hii uchambuzi wa mjadala wa matumizi ya utanzia katika riwaya teule umefanyika. Tasnifu imebaini mambo mbalimbali kama vile vijenzi vya utanzia, aina za utanzia pamoja na matukio ya kitanzia katika riwaya za waandishi teule. Aidha, matokeo yaliyotokana na utafiti huu yana umuhimu mkubwa katika tasnifu zijazo kutokana na upanuzi wa dhana ya utanzia.

## 5. 3 Hitimisho

Hitimisho linalenga kufafanua maeneo mawili ambayo ni matokeo ya utoshelevu wa mkabala uliotumika pamoja na mchango mpya wa utafiti

### 5. 3. 1 Utoshelevu wa Mkabala Uliotumika katika Utafiti

Mkabala uliotumika katika uchambuzi wa data za utafiti huu ni uhalisia. Kiini cha uhalisia ni kuelezea tapo la kifasihi ambalo huashiria uwezo wa kusawiri au kuelezea hali kwa kuzingatia uyakinifu na uhakika wa maisha. Hivyo, nadharia ya uhalisia imetuongoza katika kubainisha matukio ya kitanzia yaliyomo katika riwaya za waandishi teule. Tumechambua matukio ambayo yanasababisha hali ya huzuni kwa hadhira.

Aidha, nadharia hii imetusaidia kubaini vipengele mbalimbali vinavyoibua utanzia katika riwaya teule na kwa jamii kwa ujumla. Suala kubwa kugundua kuwa utanzia hauji bila ya kuwepo kwa sababu ambayo inasababisha hali hiyo. Hivyo, nadharia ya uhalisia imesaidia upatikanaji wa vijenzi na aina za utanzia.

Vilevile, nadharia hii imesaidia kufanya ulinganisho wa utanzia uliomo katika riwaya za waandishi teule. Kwa hiyo, imetuongoza katika kufananisha na kutofautisha utanzia uliomo katika kazi teule kwa kujiegeza katika idadi ya matukio ya kitanzia,

malengo ya utanzia, aina za utanzia pamoja na mtanzamo. Hivyo basi, ni imani yetu kwamba kwa kutumia nadharia hii, matokeo ya utafiti huu umekidhi kiwango cha ubora na uthabiti ambacho kililengwa

### 5. 3. 2 Mchango Mpya wa Utafiti

Utafiti huu ni muhimu katika uwanja wa taaluma hasa katika kutoa mtazamo mwingine wa kazi za riwaya pendwa, yaani kwa kutumia mbinu ya utanzia kuweza kuzitazama kazi hizo. Pia, utafiti huu umeongeza tafiti zilizochambua kipengele cha utanzia katika kazi za fasihi ya Kiswahili.

Aidha, riwaya pendwa zinazoonekana kutokubalika au kupewa uzito kama riwaya dhati, kutokana na maudhui yaliyomo katika riwaya hizo. Kufanyika kwa utafiti huu kutasababisha kukubalika kwa kuwa umeonesha matukio mazito yaliyomo ndani ya riwaya hizo. Hivyo, kubainisha sifa za kuwepo kwake kama ilivyo kwenye tamthiliya ambapo dhana ya tanzia hutumika.

Pia, kuibuliwa na kubainika kwa mambo matatu: Mosi, kubainika kwa utofauti wa tanzia na utanzia. Pili, kuibuliwa kwa matukio ya utanzia ambayo hujitokeza sana katika riwaya pendwa na si tamthiliya pekee. Tatu, kuibuliwa kwa aina za utanzia.

## 5. 4 Mapendekezo ya Tafiti Zijazo

Utafiti uliofanywa ulilenga kueleza matumizi ya utanzia katika riwaya pendwa za Kiswahili: Ulinganisho wa Ben Mtobwa na Hussein Tuwa. Ingawa waandishi hawa ni wawakilishi wazuri wa riwaya hizo na wametumia mbinu hii ya utanzia. Hawatoshi kutupa picha kamili ya matumizi ya utanzia katika riwaya pendwa za Kiswahili. Hivyo, bado ipo haja ya kufanya utafiti zaidi na kuhakiki riwaya za watunzi wengine mashuhuri na wasio mashuhuri.

Tasnifu hii, inapendekeza uchambuzi zaidi katika kipengele cha utanzia katika kazi za fasihi ya Kiswahili. Ambapo katika utafiti uliofanyika ulitumia riwaya nne tu za Ben Mtobwa na Hussein Tuwa, imeonekana kwamba inajitokeza kwa kiasi kikubwa katika kazi nyingine nyingi za fasihi ya Kiswahili na sio hizo tu.

Pia, tasnifu hii inapendekeza kuwa ufanyike utafiti zaidi kuhusu matumizi ya utanzia katika riwaya dhati na pendwa. Hii inatokana na kwamba matukio ya kitanzia hayapo tu katika riwaya pendwa pia, yanapatikana katika riwaya dhati. Kwa sababu riwaya zote mbili zinaandika matukio halisi yanayoitokea jamii katika maisha ya kila siku.

## MAREJELEO


Aristotle, (1965), *"Poetics" katika S. T. Dorish*, Harmondsworch, Penguin.

Bakhtin, M. M. (1981), *The Dialogic Imagination: Four Essays*, University of Texas Press, Austin.

Brereton, G. (1970), *Principles of Tragedy: A Rational Examination of the Tragic Concept in Life and Literature*, Great Britain, England.

Durey, J. F. (1993), *Realism and Narrative Modality*, Tuebingen, Gunter Navr Verlag.

Fried, M. (1987), *Realism, Writing, and Disfiguration: On Thomas Eakins and Stephen Crane*, The University of Chicago Press, Chicago.

Gromov, M. D. (2008), "Mahojiano yaliyofanyika 11/01/2008," iliyosomwa 11/08/2015 katika http://www.qucosa.de

Ibsen, H. (1879), *A Doll's House: The Collected Works of Henrich Ibsen Volume VII*, Heinemann, London.

Khamisi, S. A. M. (2007), "Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili" katika *Kioo cha Lugha*, Juzuu ya 5, TUKI, Dar es Salaam.

Kimura, E. (1991), "Mabadiliko ya Kijamii na Riwaya ya Upelelezi Tanzania," Tasnifu ya shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, (Haijachapichwa).

Kothari, C. K. (2004), *Research Methodology. Methods and Techniques*, (2nd ed), New Age International Ltd, India.

Mabala, R. (1989), "Popular Literature in Tanzania", Makala Yaliyosomwa katika *Mkutano wa 15 wa Chama cha Fasihi ya Afrika*, Dakar, Senegar.

Mackeon, R. (1947), *Introduction of Aristotle*, Random House, New York.

Madumulla, J. S. (2009), *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*, Mtule Education Publisher Ltd, Dar es Salaam.

Miller, A. (1949), *Death of a Salesman*, Carnel University, New York.

Mkubwa, C. M. (2000), “Dhana ya Utani katika Mazishi na Matanga ya Wapemba na Athari Zake kwa Jamii,” Ripoti Ndogo ya Utafiti Iliyowasilishwa kwa Mashairi ya Kutunukiwa Shahada ya Sanaa (Ualimu), Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro.

Mlacha, A. S. K. na Madumula, J. S. (1993), *Riwaya ya Kiswahili*, TUKI, Dar es Salaam.

Mtobwa, B. R. (2015), *Najisikia Kuua Tena*, Heko Publishers, Dar es Salaam.

Mtobwa, B. R. (1984), *Dimbwi la Damu*, African Publishers, Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. (1996), *Fasihi ya Kiswahili*, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. (2002), *Tanzu Tatu za Kale*, TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mushengyezi, A. (2003), *Twentieth Century Literary Theory*, Mukono Bookshop Printing and Publishing Company, Kampala.

Mutembei, A. K. (2002), “Fasihi ya Kitaifa na Fasihi ya Kiswahili ni dhana ileile?” katika *Mulika,* Juzuu ya 26, TUKI, Dar es Salaam.

Nakano, Y. (1961), *Bungaku no Joshiki*, Kadokawa, Tokyo.

Njogu, K. na Chimerah, R. (2008), *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*, Jommo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Ntarangwi, M. (2004), “Uhakiki wa Kazi za Fasihi” Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Augustino, (Haijachapishwa).

Ponera, A. S. (2014), *Utangulizi wa Nadharia: Fasihi Linganishi*, Karljamer Print Technology, Dar es Salaam.

Ponera, A. S. (2010), “Ufutuhi katika Nathari za Shaaban Robert: Maana Yake, Sababu za Kutumiwa, na Athari Zake kwa Wasomaji,” Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Rousseau, J. (1953), *Encountering Tragey*, Connell University Press, Ithaca.

Saluhaya, M. C. na Suleiman M. A. (2012), *Nadharia na Tahakiki ya Fasihi*, STC Publisher, Dar es Salaam.

Sanga, A. N. (2012), "Ujumi katika riwaya pendwa ya Kiswahili: Mifano Kutoka Kazi Teule za A. E. Musiba na M. S. Abdula," Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Shakespeare, W. (1958), *Hamlet*, Penguin, London.

Seni, D. (2015), "Fasihi Andishi" iliyosomwa 27/10/2015 katika www.academia.edu.com

Senkoro, F. E. M. K. (1981), *Maendeleo ya Riwaya ya Kiswahili*, Dar es Salaam. University Press, Dar es Salaam.

Senkoro, F. E. M. K. (1987), Fasihi na Jamii, Press na Publisity Centre, Dar es Salaam.

Senkoro, F. E. M. K. (2011), Fasihi, KAUTTU, Dar es Salaam.

Sengo, T. S. Y. (1992), "Utamaduni wa Kiswahili: Wilaya ya Kusini Unguja" katika *African Studies*, Juzuu ya 1, uk 53-79

Sewall, R. B. (2000), *The Net of Nemesis Studies in Tragic Age*, Associated University Press, England.

Soileau, C. (2006), "Money and Tragedy in the Nineteeth-Century Novel," Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi Linganishi, Chuo Kikuu cha Lousiana (Haijachapishwa).

Shivji, I.G. (2002), "Uhakiki wa Makuadi wa Soko Huria" katika *Mulika*, Juzuu ya 26, uk 93-97, TUKI, Dar es Salaam.

Snow, C. P. (1968), *The Realists: Portraits of Eight Novelists*, Macmillan, London.

Sumary, S. (2013), "Riwaya ya Upelelezi na Mabadiliko ya Kijamii: Mifano Kutoka Kazi Teule za A. E. Musiba na M. S. Abdula," Tasnifu ya Shahada ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Taasisi ya Elimu, (1996), Kiswhili Kidato cha 1 – 4. Oxford University Press, Dar es Salaam.

Tallis, R. (1998), *In Defence of Realism*, Bison Press, USA.

TUKI (2004), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es Salaam.

Tuwa, I. H. (2012), *Mdunguaji*, TuwaKadabra Production, Dar es Salaam.

Tuwa, I. H. (2014), Mazungumzo Binafsi. Yaliyofanyika 28/10/2014. saa 6:30 mchana

Tuwa. I. H. (2015), *Mkimbizi*, TuwaKadabra Production, Dar es Salaam.

Unioni, V. (1997), *Biblia: Maandiko Matakatifu,* BST, Dodoma.

UWAKI, (2013), "Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii: Mwongozo wa Kisera wa Sekta ya Afya wa Kuzuia na Kupambana na Ukatili wa Jinsia," iliyosomwa 28/01/2016 katika www.healthpolicynitiative.com

Wafula, R. M. & Njogu K. (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, The Jomo Kenyata Foundation, Nairobi.

Wamitila, K. W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na vipengele vyake*, Phoenix Publishers Limited, Nairobi.

Wamitila, K. W. (2003), *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*, Focus Books, Nairobi.

Wehmeier, S. (2006), Oxford Advanced Learner's Dictionary, Oxford University Press, USA.

Wellek, R. (1961), *The Concept of Realism in Literary Scholarship*, Neophiloques Limited, London.

Villanueva, D. (1997), *Theories of Literary Realism*, State University, New York.

## VIAMBATISHO

### A. Miongozo ya Usaili na Udurusu

### A. 1 Mwaongozo wa Usaili kwa Wataalamu wa Fasihi

Utafiti huu unahusu matumizi ya utanzia katika maandiko ya Ben Mtobwa na Hussein Tuwa. Lengo la utafiti ni kuyaibua matukio ya kiutanzia pamoja na kujua jinsi unavyotokea na mabadiliko ambao utanzia unayapitia katika fasihi na jamii ya Watanzania kwa ujumla. Aidha, utafiti unalenga kutaka kujua aina za utanzia uliomo katika maandiko ya waandishi hawa teule zinahusiana au kutofautiana.

1. Utanzia ni hali ya huzuni, masikitiko, maumivu pamoja na masononeko. Kwa maoni yako, unaielewaje dhana ya utanzia?
2. Unafahamu nini kuhusu chimbuko la utanzia katika jamii ya Watanzania?
3. Unadhani kuna aina mbalimbali za utanzia? Kama ndio zitaje.
4. Ni kazi ipi/zipi za Hussein Tuwa au Ben Mtobwa ambazo umewahi kuzisoma au kuzihakiki au kuzitafiti?
5. Ni tukio au matukio gani ya kitanzia yaliyomo katika kazi za waandishi hawa wawili ambayo unayakumbuka? Kwa maoni yako, matukio hayo yana maana gani?
6. Una maoni gani kuhusu utumiaji wa mbinu ya utanzia katika riwaya pendwa za Kiswahili?

### A. 2 Mwongozo wa Usaili kwa Mwandishi Hussein Tuwa

1. Naomba kujua historia yako kwa ufupi.

2. Unaelewa nini kuhusu riwaya pendwa?

3. Kuna aina ngapi za utunzi? Zitaje

4. Wewe unatumia aina ipi? Na kwa nini hiyo?

5. Je unazipataje mbinu za uandishi? Na zipi unazozitumia zaidi?

6. Nini maana ya utanzia?

7 Unaelewa nini kuhusu mbinu ya utanzia katika uandishi wa kazi za fasihi?

8. Kuna sababu zipi zilizokufanya kutumia mbinu ya utanzia katika riwaya zako za *Mkimbizi…?*

9. Kuna umuhimu gani wa matumizi ya utanzia katika riwaya pendwa za Kiswahili?

10. Je, umewahi kusoma kazi za waandishi wengine hususani Ben Mtobwa?

11. Waandishi gani wa riwaya unaowakubali? Kwa nini?

12. Je, una mpango gani kwa hadhira yako kwa siku za usoni?

**A. 3 Mwongozo wa Usaili kwa Familia ya Ben Mtobwa**

1. Naomba hueleze kwa ufupi kuhusu jina na umri wako.

2. Je unamjua Ben Mtobwa? Kama ndivyo, eleza umjuavyo.

3. Ni jambo/mambo gani ambayo Beni Mtobwa upendelea kufanya?

4. Ni jambo/mambo gani ambayo Ben Mtobwa aliyapinga au kuyachukia?

5. Umeshawahi kusoma kitabu/vitabu vyovyote vya Ben Mtobwa? Kama ndio ni kipi/vipi?

6. Je unakumbuka tukio/matukio yoyote ya huzuni katika kitabu hicho/hivyo? Kama ndio ni yapi?

7. Je unakumbuka tukio/matukio yoyote ya huzuni ambayo yalimtokea Ben Mtobwa Kama ndio ni yapi?

**B. Barua ya ridhaa ya kufanya utafiti**

**CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM**
**TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI**

S.L.P. 35110 Dar es Salaam
Simu Na:Mkurugenzi: 2410757
Simu ya Jumla: 2410500-8 Tawi. 2647
Fax: 022 - 2410334

Barua-e: tuki@ikr.udsm.ac.tz
ikr@udsm.ac.tz
Tovuti: www.udsm.ac.tz/tuki
www.udsm.ac.tz/ikr

Kumb: TATAKI/B 116

Tarehe: 10.03.2016

Kwa: Wana-TATAKI
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

**YAH: KUKUSANYA DATA KUTOKA KWA WATAALAMU WA FASIHI TAASISINI**

Tafadhali husika na somo hilo hapo juu.

Napenda kumtambulisha Bi. Kuruthum Mazongela kuwa ni Mwanafunzi wa Uzamili katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Hivi sasa yupo katika hatua ya kukusanya data kwa ajili ya utafiti. Mada ya utafiti ni 'Matumizi ya Utanzia katika Riwaya Pendwa za Kiswahili'. Moja ya maeneo ya ukusanyaji data ni Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Tafadhali unaombwa kutoa msaada atakaouhitaji kuhusiana na utafiti wake.

M. Mbinda
**Kny: Mkurugenzi, TATAKI**

nk: Mkurugenzi, TATAKI
nk: Mkurugenzi Mshiriki, TATAKI
nk: Mkuu wa Idara ya LUKII
nk: Mkuu wa Idara ya FAMU

**C. Picha Mbalimbali**

C. 1 Picha Zinazohusiana na Ben Mtobwa



**Mwandishi Ben Mtobwa enzi za uhai wake (Utafiti, 2016)**



**Mtafiti aliyeshika picha pamoja na watoto wa Ben Mtobwa, Neema Mtobwa (katikati) na Comfort nyumbani kwao Bunju (Utafiti, 2016).**



**Picha ya kaburi la Ben Mtobwa liliopo nyumbani kwake Bunju (Utafiti, 2016).**

**C. 2 Picha Zinazohusiana na Hussein Tuwa**



**Mwandishi wa riwaya Hussein Tuwa (katikati) pamoja na watafiti, Happy Bitababaje (kushoto) na Kuruthumu mazongela wakati wa mahojiano nyumbani kwake Kimara (Utafiti, 2016).**




**Mtafiti pamoja na wadogo wa Hussein Tuwa wakati wa mahojiano yaliyofanyika dukani kwa Hussein Tuwa Kinondoni (Utafiti, 2016).**

**B. 3 Picha Nyinginezo**



**Mtafiti pamoja na Prof. Mutembei wakati wa mahojiano yaliyofanyika Machi 15, 2016 Dar es Salaam. Mutembei ni mhadhiri wa Fasihi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam 15/03/2016 (Utafiti, 2016).**




**Mtafiti pamoja na Bi Eliza Mahenge wakati wa mahojiano yaliyofanyika Machi, 12 2016 Dar es Salaam. Bi Mahenge ni mhadhiri-msaidizi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Utafiti, 2016).**